SportPesa
TZS. 482,274,020
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Kesi** ya Mbowe tuhuma ugaidi kunguruma leo

UKURASA 3

KCOM
Tunafunga **GPS** kwenye gari, pikipiki na TV



TUPIGIE: +255 624 279 186
+255 652 000 020
@kcom.tz

Ijumaa Septemba 10, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 10

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580699
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# KIZAAZAA KARIAKOO

• **Machinga** avua nguo kutetea meza isichukuliwe, RC atoa tamko... *Endelea ukurasa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akizungumza na wafanyabiashara wadogo maarufu Machinga katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutokea vurugu za kogombea maeneo ya kufanyia biashara baina yao. **Picha ndogo:** Akikagua wafanyabiashara hao walivyopanga bidhaa zao kwenye njia za waenda kwa miguu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Sabaya kortini rushwa, uhujumu uchumi

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

## Begi kubwa la mwanafunzi

• **Hadhari** yatolewa uzito, madaktari waonya maradhi...*Uk.4*

**MICHEZO** **MANARA 'AJILIPUA' SIMBA KWA YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kizaazaa chaibuka sokoni Kariakoo

**Na Waandishi Wetu**

NI Kizaazaa. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na vurugu za wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, zilizotokea eneo la Sunderland, Kariakoo jijini Dar es Salaam ambao walikuwa wakigombea maeneo sokoni hapo kwa ajili ya kufanya biashara.

Vurugu hizo zilisababisha mmoja wa machinga hao kuvua nguo na kubaki utupu.

Video fupi iliyosambaa mitandaoni jana asubuhi, ilimwonyesha kijana akiwa mtupu amebeba meza za machinga na kuzipanga kwenye eneo ambalo vijana hao walitaka zikae ili wafanye biashara.

Wakati wa vurugu hizo baadhi ya vijana walionekana wakipigana wenyewe kwa wenyewe na wengine wakirushiana meza ambazo hutumia kupangia bidhaa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Ilala, Debora Magiligimba, alipoulizwa na Nipashe kuhusiana vurugu hizo zilizosababisha kijana huyo kukaa utupu mbele ya watu, alisema msemaji wake ni Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro.

Kamanda Muliro alipoulizwa, alisema, "Kitendo kilichofanyika Kariakoo ukitembelea maeneo kama bandarini kama ni mgeni utaona ni vituko, lakini kwa wenyeji kwao ni vitu vya kawaida. Hata kwenye maeneo ya uvuvi hutokea, kwa mgeni ataona si vya kawaida.

"Kariakoo kuna mchanganyiko wa vijana wengi wenye rika tofauti na wanaotoka kwenye familia tofauti. Utakutana na matukio ambayo wewe ukiyaona utashangaa lakini wao hawashangai."

Gazeti hili lilipotaka kujua kama kuna watu wanashikiliwa kutokana na vurugu hizo, Kamanda Muliro alisema jeshi lilichofanya ni kuhakikisha eneo hilo hali inakuwa shwari na shughuli zinaendelea kufanyika.

Baada ya tukio hilo kutokea, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ambaye alifika eneo hilo, alipiga marufuku ufanyaji wa biashara kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara baada ya utaratibu huo kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani na ongezeko la ajali.

"Ninatoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala kufanya kikao na wafanyabiashara Jumatatu (Septemba 13) na kuainisha maeneo ya kuwapeleka waliovamia hifadhi ya barabara kwani wanasababisha usumbufu kwa wananchi wengine," alisema.

Makalla alisisitiza kuwa njia za watembea kwa miguu lazima zibaki wazi na wamebaini kuna watu ndani ya serikali wanawauzia machinga maeneo hayo kwa kuwahesabia hatua ambazo hulipa Sh. 200,000 hadi Sh. 300,000.

Pia aliwaagiza wakuu wa wilaya zote mkoani humo kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri wa wafanyabiashara hao na kusisitiza kuwa Kariakoo wanaweza kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua baadhi ya mitaa kwa ajili ya kufanya biashara utokanao na ufinyu wa maeneo.

Kiongozi huyo alisema tathmini aliyofanya amebaini kuna ufanyaji biashara holela ambao unawanyima haki za msingi watembea kwa miguu na kuagiza manispaa ziweke vibao vya kuzuia biashara kwenye hifadhi ya barabara na zile za waenda kwa miguu.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara, Steven Lusinde, alisema kanzidata ambayo wameitengeneza ili kuwatambua wafanyabiashara sokoni hapo hawaitambui hao waliofanya vurugu.

●**Imeandaliwa na Romana Mallya na Maulid Mmbaga**

## Watano wafariki ajali za pikipiki

**Na Waandishi Wetu**

WATU watano wamefariki dunia katika matukio mawili tofauti ya ajali za pikipiki yaliyotokea Nzega, mkoani Tabora na Dar es Salaam.

Katika tukio la Nzega watu watatu waliokuwa wamepakizana mshikaki kwenye pikipiki wamefariki dunia papo hapo kwa kugongana uso kwa uso na Fuso lenye namba ya usajili T507 BCF.

Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, Safia Jongo, alisema vijana hao wanakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 15 hadi 18 na waligongwa wakiwa wamebebana kwenye pikipiki.

Alisema ajali hiyo ilitokea Septemba 7, majira ya saa 12 jioni katika eneo la Tazegwa, barabara itokayo Nzega Mjini kuelekea mkoani Tabora.

Aidha, alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa pikipiki aliyekuwa akitokea Nzega Mjini na kuelekea katika kitongoji cha Shagiro na alipojaribu kuyapita magari mawili na kabla hajafanikiwa kuyapita alikutana na Fuso hilo na kuwagonga.

Kamanda Safisa alisema pikipiki hiyo ilikuwa katika mwendo wa kasi na ajali hiyo imetokana na kutokuwa makini barabarani. Aliwataja watu waliofariki kuwa ni Paulo Petro, Rubeni Jogi na mwingine alitambulika kwa jina moja la Nasoro.

Aidha watu wawili wamefariki dunia baada ya pikipiki waliyokuwa wakiitumia kusafiria kugongana na basi la mwendo wa haraka eneo la Lumumba, jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro aliwataja waliofariki dunia kuwa ni dereva wa pikipiki Sami Riyaz Khan (17), mkazi wa Gerezani na abiria wake, Patrick Chohan (16).

Alisema chanzo cha ajali hiyo ambayo ilitokea juzi usiku ni dereva wa pikipiki kupita kwenye taa nyekundu za kuongezea magari zilizopo Lumumba.

Alisema waliokufa walikuwa kwenye pikipiki yenye namba za usajili MC 663 CDX aina ya Boxer ambayo iligongana na basi la mwendokasi lenye namba za usajili T 880 DGV aina ya Golden Dragon lililokuwa likitokea Kimara kuelekea Kivukoni.

●**Imeandaliwa na Halima Ikunji (Tabora) na Romana Mallya (Dar es Salaam)**



Mratibu wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Josephine Arnold, akitoa maelezo wakati wa semina ya siku moja ya wabunge wanawake jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Sabaya kortini mashtaka ya uhujumu, rushwa na matumizi mabaya madaraka

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MKUU wa zamani wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake sita, wamepandishwa kizimbani na kusomewa mashtaka matano.

Walisomewa mashtaka hayo jana katika kesi ya uhujumu uchumi mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akisoma mashtaka, wakili huyo alidai kwamba katika shtaka la kwanza, washtakiwa waliongoza genge la uhalifu kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa kwamba Januari 22, mwaka huu, washtakiwa hao kwa pamoja katika maeneo tofauti ya Jiji la Arusha, wakiongozwa na Sabaya akiwa mtumishi wa serikali kwa nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, walifanya vitendo vya uhalifu kwa kujipatia Sh. milioni 90 kwa manufaa yao.

Shtaka la pili linamhusu Sabaya ni juu ya kujihusisha na vitendo vya rushwa kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B, 2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019..

Ilidaiwa kwamba Januari 22, mwaka huu, katika maeneo ya kwa Murombo jijini Arusha, Sabaya alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumtaka Francis Mroso kumpatia Sh. milioni 90 kwa kumshinikiza ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo juu ya madai ya ukwepaji kodi.

Wakili huyo wa serikali alidai kuwa shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili Sabaya peke yake kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Alidai kuwa Januari 22, mwaka huu, Sabaya akiwa katika maeneo ya kwa Morombo, alijipatia Sh. milioni 90, kutoka kwa Francis Mroso, ili asitoe taarifa za jinai za madai ya ukwepaji kodi dhidi yake.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka na linamkabili Sabaya peke yake ambalo ni kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Ilidaiwa Januari 22 mwaka huu, katika eneo la kwa Murombo, Sabaya alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, kwa kumtishia Francis Mroso, kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi, kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu cha 15(9) cha Sheria ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa lengo la kujipatia kiasi hicho cha fedha.

Wakili Tersila alidai kwamba shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba kinyume cha kifungu 12 (D),13(1A) cha Sheria ya Utakatishaji Fedha Sura ya 423 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Alidai kuwa Februari 22, mwaka huu, Sabaya kwa kushirikiana na wenzake, katika eneo la kwa Murombo, walijipatia Sh. milioni 90 huku wakitambua kwamba kufanya hivyo ilikuwa zao la vitendo vya rushwa.

Baada ya Wakili wa serikali kumaliza kuwasomea mashtaka hayo, Sabaya na wenzake walikana mashtaka yanayowakabili.

Wakili huyo wa serikali, aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa kwa shauri hilo ili kuwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao.

Hakimu Kisinda, baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka yanayowakabili, aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 16, mwaka huu, itakapotajwa kwa washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Washtakiwa hao, wamerudishwa rumande katika mahabusu ya Gereza Kuu la Kisongo kwa kuwa kesi hiyo haina dhamana.

## HABARI KITAIFA




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa Tamasha la Vyakula na Raslimali za Baharini, jijini Zanzibar jana. Benki ya NMB ni wadhamini wakuu wa tamasha hilo litakalofanyika Oktoba 8-9. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud na Meneja Msimamizi wa Biashara NMB Zanzibar, Abdallah Duchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya Mbowe ya ugaidi kuanza leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi leo inatarajia kuanza kusikiliza kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Kesi hiyo itaanza kusikilizwa mbele ya Jaji Mustapha Siyani baada ya Jaji Elinaza Luvanda kujitoa.

Kwa mujibu wa hati ya wito iliyotolewa na kusainiwa na Naibu Msajili wa mahakama hiyo, kesi itaanza kusikilizwa kwa washtakiwa kusomewa mashtaka yao na maelezo ya awali dhidi ya mashtaka yanayowakabili.

Kabla ya kuombwa kujitoa Jaji Luvanda alitoa uamuzi wa mapingamizi ya upande wa utetezi uliokuwa ukidai hati ya mashtaka ina kasoro.

Alikubaliana na hoja moja ya pingamizi na kutupilia mbali hoja mbili kwa kusema msingi wa pingamizi ni makosa yaliyofunguliwa chini ya kifungu namba 4(3) cha Sheria ya ugaidi namba 21 ya mwaka 2002, haikueleza malengo wakati ndio msingi wa makosa ya ugaidi kwa shtaka namba 1,4,6.

Alisema kwa maoni yake hoja hiyo inachukua muda mrefu, marejeo yalipaswa kufanywa katika hansard za Bunge, kuona michango ya wabunge wakati sheria hiyo inatungwa kuona kama walitoa tafsiri ya ugaidi bila kuhusisha itikadi za dini na siasa.

"Majibu yanapatikana katika hansard, sipendi kuhitimisha katika hatua za awali, itafutiwe hoja nzito zaidi itatolewa uamuzi huko baadaye,"alisema Jaji Luvanda.

Jaji Luvanda alisema Mahakama inakubaliana na hoja moja ya upande wa utetezi kwamba shtaka namba 1,4, 6 yaliyofunguliwa chini ya kifungu namba 4(3) cha Sheria ya ugaidi ilikuwa ni sharti kutumia maneno yaliyolengwa chini ya kifungu hicho.

Alisema anakubaliana na hoja ya Wakili Peter Kibatala kwamba, ili kuweka tofauti hayo maneno yanaweka mpaka baina ya makosa ya ugaidi na makosa mengine ya jinai.

Aliamuru upande wa Jamhuri kufanyia mabadiliko shtaka namba 1,4 na 6 na alipojitoa na Jaji atakayepangiwa ataanzia alipoishia.

Katika shauri hilo Jamhuri inawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Kidando Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.

Upande wa utetezi unawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamo na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Katika shtaka la kwanza wanadaiwa wote, walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi, 2020 katila hoteli ya Aishi iliyopo Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na kutaka kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Sabaya.

Shtaka la tatu, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo aliwawezesha kifedha Halfani Adamu na Ling'wenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, Katiba, uchumi na sifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shtaka la nne wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi.

Shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, 2020 eneo la Rau alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger.

Mshtakiwa Halfani katika shtaka la sita anadaiwa Agosti 10, 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambazo ni suruali moja ya JKT, pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana, koti la mvua, jaketi, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

# Kampuni 9 za mafuta zatozwa faini ya bil.5/-

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limezitoza faini ya jumla ya Sh. bilioni 5.1 kampuni tisa za mafuta zilizojenga vituo vya mafuta bila kuwa na vyeti vya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA).

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msako unaoendelea kuhusu vituo vya mafuta visivyo na vyeti hivyo.

Alisema vituo vyote hivyo vinapaswa kuhakikisha vinalipa faini hiyo ndani ya siku 14 kuanzia leo na kutaka wengine wanaojijua kwamba hawana vyeti hivyo kujisalimisha wenyewe kwenye baraza kabla hawajafikiwa waliko.

Dk. Gwamaka alisema kwenye msako unaoendelea kwenye mikoa yote nchini wamegundua vituo 393 vya mafuta ambavyo havina vyeti vya EIA, lakini vinaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Alizitaja kampuni hizo ni Oryx yenye vituo 15 ambavyo havina vyeti vya EIA ambapo kampuni imetozwa faini ya Sh. milioni 750.

Alitaja kampuni nyingine ni PUMA yenye vituo 22 ambapo vyote vimetozwa faini ya Sh. bilioni 1.1, kampuni nyingine ni TOTAL yenye vituo 16 ambayo imetozwa faini ya Sh. milioni 800.

Dk. Gwamaka alitaja kampuni nyingine ni CAMEL Oil yenye vituo sita, ambayo imetozwa faini ya Sh. milioni 300, GBP yenye vituo 10 iliyotozwa Sh. milioni 500 na GAPCO yenye vituo nane iliyotozwa faini ya Sh. milioni 400.

Kampuni zingine ni Ester Oil yenye vituo tisa ambayo imetozwa faini ya Sh. milioni 450, OIL COM vituo 12 imetozwa faini ya Sh. milioni 600 na TSN yenye vituo vine imetozwa faini ya Sh. milioni 200.

"Hawa niliowataja ni baadhi tu kwa sababu msako unaendelea nchi nzima na tutaendelea kuwatangaza na faini wanazopewa kila tunapowabaini, maana mbali na kukosa vyeti vya EIA, wanaikosesha serikali kodi ambayo wangepeswa kuilipa," alisema.

Jumatatu, NEMC iliitoza ya Sh. bilioni 3.3 Kampuni ya Mafuta ya Lake Oil inayotuhumiwa kujenga vituo vingi vya mafuta maeneo mbalimbali nchini bila kuwa na EIA.

NEMC ilimtaka mmiliki wa kampuni hiyo kulipa faini hiyo ndani ya siku 14 na asipofanya hivyo itatumia sheria kuvifungia vituo vyake vyote 66 nchini.



## RIPOTI MAALUM

# BEGI KUBWA LA MWANAFUNZI

## •Wakati hadhari kuu ni uzito, madaktari waonya maradhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ELIMU ya shule sasa imepiga hatua kulinganisha na nchi ilikotoka. Wingi wa shule za umma na binafsi ni uthibitisho tosha wa mafanikio yalifikiwa katika Sekta ya Elimu nchini.

Hata hivyo, maendeleo ya sekta hiyo yamekwenda sambamba na kuibuka kwa mitindo mipya ya maisha, ukiwamo unaotawala sasa wa mabegi ya kila mtindo miongoni mwa wanafunzi.

Hapo ndipo panaanza 'kanuni sheria' kuwataka wanafunzi kuwa na mabegi makubwa, wakibebea mahitaji ya shule kama madaftari makubwa aina ya kaunta sambamba na vitabu vikubwa vinavyopendekezwa kama kamusi mbili za Kiingereza na Kiswahili.

'Kanuni sheria' hiyo ya watoto kubebeshwa begi zito likijumuisha mahitaji kama maji, sasa ni mtindo kwa karibu shule zote unaowapa wanafunzi mateso, hali kadhalika kukaribisha maradhi.

Ushuhuda wa madhara kuelekea mateso unajitokeza zaidi kwa watoto wadogo kama wa darasa la tatu hadi la tano, hata kuchukua sura ya maradhi.

Wakati wengi wakidhani hali hiyo ni ya nchini pekee kulingana na mageuzi ya soko huria, kuna ushahidi wa yanayojiri kwa picha ileile katika nchi jirani.

Tayari wataalamu wa afya wana angalizo lao la hatari kubwa kimwili zaidi ya maumivu ya kawaida.

"Dada ninaomba unisaidie begi," binti mwenye umri wa miaka tisa anasikika ndani ya daladala akiomba kusaidiwa kubeba begi lenye vifaa vyake vya shule.

Udadisi wa Nipashe uliofadhiliwa na Taasisi ya Habari ya CHIMBUA Communication, unabaini binti huyo aliyejitambulisha kwa jina la Amina, ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Nkuhungu mjini Dodoma.

Madaftari, vitabu, chupa yenye maji ya kunywa pamoja na mahitaji mengine ya shule, vyote vimelifanya begi lake kuwa zito, hivyo kugeuka adha kwake kutokana na taratibu za daladala zinazozuia wanafunzi kuketi kwenye viti vya gari.

Katika majumuisho ya mazungumzo na binti huyo, Nipashe inabaini ubebaji wa mabegi yenye uzito mkubwa miongoni mwa wanafunzi, unasababisha adha kubwa dhidi ya kundi hilo na hata kuhatarisha usalama wa zao. Zawadi Joseph, mmoja wa wakazi wa Nkuhungu mjini Dodoma, ana ushuhuda wa kinachowakabili wanafunzi, akiuwasilisha:

"Mwanangu Christian ana umri wa miaka tisa na yuko darasa la nne sasa. Mara kwa mara alikuwa analalamika maumivu ya mgongo anapokwenda kulala.

"Baada ya kumfuatilia kwa muda, nilibaini ni uzito wa begi ndio mzizi wa tatizo linalosababisha maumivu hayo.

"Nilikwenda shuleni ili nijue labda ile sehemu anayoketi sio nzuri, lakini wakati ninatafakari, mwalimu wake aliniita na kuniambia 'mtoto anaelemewa sana na begi, ninaomba uwe unamsaidia'.

"Kwa kuwa kuna umbali mrefu kwenda shule, nimelazimika kuwa ninamsindikiza na kumbebea begi lake. Simsikii tena akilalamika maumivu ya mgongo.

"Kabla ya kuchukua uamuzi huo, nilimpeleka mwanangu hospitali mbalimbali, lakini maumivu bado yaliendelea kumsumbua.

"Yaani begi lake lina madaftari mengi, hebu fikiria kuna daftari la hesabu namba moja na mbili, jumlisha na masomo mengine yaliyopo, bado hajaweka vitabu vyake, chupa ya maji... begi linakuwa zito sana."




**KUTOKA KWA WANAFUNZI**

Josephina Almasi, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Amani anasema analazimika kubeba vitabu na madaftari yote kwa kuwa wakati mwingine hujisomea shuleni wakati wa mapumziko.

"Lakini hatusomi kwa kufuata ratiba, walimu wanatutangazia 'mje na madaftari yote'. Wakati mwingine mwalimu aliyepangwa anaweza kupata dharura akaingia wa somo lingine, ambaye hayupo kwenye ratiba ya siku husika," anasema.

Anthony Silwa, mwanafunzi mwingine katika shule hiyo, anabainisha kuwa baadhi ya walimu wakimkuta hana daftari la somo husika, hupewa adhabu, hivyo kulazimika kubeba madaftari na vitabu vyote vya shule ili kuepuka adhabu.

**KENYA NAKO SHIDA**

Mwanandishi wa habari, Dancan Maiche, kutoka Kenya, anabainisha kuwa ubebaji mabegi makubwa miongoni mwa wanafunzi kwa sasa unashuhudiwa pia katika nchi hiyo jirani.

Anasema hali hiyo ipo hasa kwa wanafunzi wa shule za umma ambao hulazimika kubeba madaftari na vitabu vyao kila siku ili visiibwe shuleni. Maiche anasema wanafunzi wa shule binafsi huacha vitu vingi shuleni, wakibeba madaftari mawili au matatu pamoja na shajara inayoonesha kazi zinazopaswa kufanyika nyumbani.

"Wanafunzi wa shule za umma hawana madawati ambayo yana uwezo wa kufungia vifaa vyao tofauti na wa shule binafsi ambao madawati yao yanafungika," anasema.

Hata hivyo, mwanahabari huyo anafafanua kuwa Kenya sasa ina mtaala mpya ambao ulianza kutekelezwa mwaka jana, ukiweka masharti kwa wazazi kununua madaftari na vitabu vingi kwa kuwa masomo yameongezeka.

"Unajua mtaala uliopita mtoto alikuwa anasoma ili kufanya mtihani, huu mtaala wa sasa unamsaidia pia kupata stadi za maisha, unaweza kuta amepewa kazi za nyumbani kama kutengeneza fagio," anasema.

Maiche anashauri serikali na wadau kuangalia namna ya kuwa na madawati yanayofungika ili kumwondolea mzigo mwanafunzi.

**UTAFITI**

Utafiti uliofanywa na Chemba ya Biashara India mwaka 2018, ulibainisha ubebaji wa mabegi mazito kwa watoto ni hatari na unaathiri misuli laini inayokua.

Ufuatiliaji wa Nipashe kuhusu kadhia hiyo umebaini mabegi hayo ni tishio kwa afya za watoto hasa wanafunzi wa madarasa ya mtihani, yaani darasa la nne na la saba.

Nipashe haikufanikiwa kupata mwongozo wowote uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu aina ya mabegi yanayopaswa kubebwa na wanafunzi.

Nipashe pia imebaini wengi wao hubeba mabegi yaliyosheheni vitu mbalimbali vikiwamo vitabu, madaftari ya masomo ya kiada na ya ziada yenye uzito unaokadiriwa kuwa kati ya kilo sita na 10 ambao ni mkubwa kulinganishwa na uwezo wa miili yao.

**WATAALAMU WA AFYA**

Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa mkoani Dodoma, Julieth Kabengula, anaonya kuwa ubebaji wa mabegi hayo husababisha kupinda kwa mgongo na kuumwa mgongo, tatizo ambalo hujitokeza katika ukuaji wa mtoto.

"Shule zinasababisha madhara haya kwa watoto... wanatakiwa kupewa ratiba ili waweze kubeba vitabu vitakavyotumika siku hiyo. "Zamani sisi wakati tunasoma tulikuwa tunajua masomo ya siku husika na tunabeba kulingana na ratiba.

"Sasa kama wanaona ratiba zao zinabadilika, ni vyema kutengeneza makabati ili kuwapunguzia mzigo watoto ili arudi na daftari alilopewa kazi za nyumbani tu.

"Hili ni tatizo. Ni muhimu kuchukua hatua kulingana na ushauri tunaotoa wataalamu. Tusipofanya hivi huko baadae tutakuwa na watoto wenye tatizo la kupinda kwa migongo na ikitokea hivyo, hilo tatizo linaweza pia kuathiri mishipa ya fahamu," anaonya.

Hata hivyo, Dk. Julieth anafafanua kuwa tatizo hilo mara nyingi linachukua muda mrefu kuonyesha madhara ya wazi.

Mtaalamu wa Mazoezi Tiba ya Mifupa mkoani Arusha, Susan Kanora, ana angalizo kwa wazazi kuhakikisha watoto wao hawabebi mabegi yenye uzito mkubwa.

"Unakuta mtoto mdogo anabeba uzito mkubwa kwenye mgongo wake, kile kitu kinaleta athari kubwa katika kukua kwake kwa kuwa uti wa mgongo unashindwa kuhimili uzito wa mzigo ambao mtoto anabeba.

"Mtoto anayebeba begi zito, huwezi kumkuta amebeba kwa kunyooka, siku zote utamkuta anatembea ameinama kwa sababu ya uzito.

"Na hupata maumivu makali baada ya kushusha begi wakiwa darasani, unaona kabisa utulivu wa mtoto kusikiliza masomo haupo, anakuwa anasikilizia maumivu ya begi.

"Maumivu yake yanaanzia shingoni na kadri anavyobeba anaendelea kukomaa na kusababisha kupata shida kubwa.

"Kuna mshipa ambao unahitaji kukua kwa mtoto, unapokuwa unabanwa na uzito na kubana misuli midogo midogo, humsababishia mtoto kushindwa kunyooka.

"Wagonjwa wangu wengi kwa sasa ni watoto, tunawafanyia mazoezi tiba, lakini si rahisi kwa kila mzazi kubaini tatizo, mwingine anahisi mtoto ni mzembe kumbe anasumbuliwa na misuli. "Wengine wakibeba begi wanaelemea upande mmoja, hivyo matibabu yake unabaini mgongo umepishana, mwingine anatembea kwa kuinama. Tunatoa matibabu na kushauri kama kuna vitu vizito anabeba kwenye begi aviache," anafafanua.

Mtaalamu huyo anashauri shule kuweka kabati kwenye madarasa kwa ajili ya kutunza vifaa vya watoto au kuzuia wanafunzi kubeba mabegi ili kusaidia kuepusha shida za mgongo wanazopata watoto.

"Walimu pia wanapaswa kuliangalia suala hilo kwa kuweka ratiba ambazo zitazingatiwa na kupunguza mzigo kwa mtoto," anashauri.

**WADAU WA ELIMU**

Mchambuzi wa masuala ya elimu, Mwalimu Gradius Ndyetabula, anaunga mkono hoja ya mshauri huyo, akishauri kuwe ratiba ya masomo yanayofundishwa kwa siku husika na walimu waheshimu ratiba hiyo.

Hata hivyo, anakosoa mfumo wa elimu nchini unaomlazimisha mwanafunzi wa darasa la saba kukumbuka kila alichosoma kuanzia chekechea ili awe na sifa za kufanya vizuri na kufaulu mtihani wake wa mwisho.

Mwalimu Samson Thomas kutoka moja ya shule binafsi mkoani Dodoma, anasema wapo baadhi ya wanafunzi hubeba mabegi makubwa kama mtindo wa kisasa wa ubebaji licha ya kuwa kunakuwa na madaftari machache ya kazi za nyumbani.

"Shule yetu ni ya mchepuo wa Kiingereza na ina ratiba na shajara ambazo kila siku mwalimu anajaza mwenendo wa mtoto, mzazi anaweza kumwekea mwanawe madaftari kulingana na masomo ya siku husika, lakini kuna hulka tu ya wanafunzi kwa sasa kupenda kubeba mabegi makubwa," anasema.

Mratibu wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TenMet), Cathleen Sekwao, anashauri ianzishwe kampeni aliyoiita ya kumtua mtoto begi mgongoni ili kuhamasisha shule zisimamie ubebaji wa mabegi kulingana na masomo ya siku husika tu.

Anasema baadhi ya walimu wanasababisha watoto kubeba madaftari na vitabu vingi kutokana na tabia ya kuingia darasani bila kufuata ratiba.

Dk. Wilberfoce Meena kutoka Shirika la HakiElimu, anasema kuna tatizo kwenye mtaala wa elimu nchini kwa kuwa wanafunzi wanasoma kwa kufikiria mitihani, akishauri mfumo wa elimu uangaliwe ili uwe jumuishi na kuondoa kero zilizopo.

HABARI KITAIFA

# ATCL yaja na tiketi za kibubu

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMPUNI ya Ndege Tanzania (ATCL), imezindua mpango wa kulipia tiketi kwa awamu uitwao kibubu wenye lengo la kuwarahishia Watanzania kutumia huduma za kampuni hiyo katika mtandao wa safari za nchini na kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Saalam kuhusu huduma hiyo, Meneja wa Mtandao na Usimamizi wa Mapato wa ATCL, Edward Mkwabi, alisema mteja ataweza kufanya maandalizi ya safari mtandaoni ama kufika katika ofisi za ATCL.

"Mpango huu utawaruhusu walengwa kulipia tiketi zao kidogokidogo na katika awamu ya mwisho ya kukamilisha malipo yote mteja atapewa tiketi yake. Mpango huu unatarajiwa kuleta unafuu katika kulipia gharama za usafiri wa ndege pia kuongeza idadi ya abiria watakaotumia huduma zetu," alisema Mkwabi.

Alifafanua kuwa abiria atatakiwa kufanya maandalizi ya safari kisha atalipa kwa awamu ya kwanza Sh. 50,000 katika ofisi za ATCL, kisha atapewa stakabadhi ya malipo kwa kila awamu atakayolipa inayomaanisha kupokelewa kwa malipo yake.

Alisema mteja atapewa tiketi yake baada ya kukamilisha malipo yote ya nauli ya safari husika.

"Pia tutatekeleza mpango huu kwa kupokea malipo kupitia benki na taasisi za fedha mbalimbali. Kwa njia hii msafiri ataingia mkataba moja kwa moja na benki au taasisi ya fedha tutakayoingia nayo mkataba," alisema.

Mkwabi alisema baada ya mteja kufanya maandalizi ya safari atajulisha benki au taasisi ya fedha husika nayo italipa moja kwa moja fedha yote ya tiketi ATCL, kwamba mteja atailipa benki hiyo fedha kidogo kidogo kulingana na makubaliano yao.

Kuhusu mteja kushindwa kumaliza fedha za malipo, alisema: "Mteja atakaposhindwa kumaliza kiasi cha nauli na akitaka kurudishiwa pesa alizolipa, masharti ya daraja alilofanya maandalizi ya safari ya tiketi husika yatafuatwa ili kuweza kurudishiwa kiasi cha pesa."

Alisema siku zijazo pia huduma hiyo itapatikana kwenye mitandao ya simu, mteja ataweza kulipia tiketi kidogokidogo kupitia simu yake hadi atakapomaliza awamu ya mwisho ya malipo na kupata tiketi yake moja kwa moja kupitia mtandao atakaochagua.

Naye Ofisa Masoko wa ATCL, Grace Magubo, alisema mpango wa kulipa tiketi kidogokidogo pia umekuja na promosheni ya zawadi, kwamba mteja atayeleta wateja wengine watano atapewa punguzo la nusu bei ya tiketi.

# Mapya yaibuka biashara ya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, kuwarejesha watoto 11, waliokuwa wanadaiwa kuwa walitoroshwa na kuuzwa kwa wafugaji wilayani Mbarali, ili watumike kuchunga mifugo, baadhi ya wazazi wa watoto hao wameibuka na kudai waliridhia watoto wao kwenda kufanya kazi hiyo.

Septemba 7, mwaka huu, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, akizungumza na wandishi wa habari hizi, alisema Jeshi hilo liliwakamata watu wawili kwa tuhuma za kuwaiba watoto hao 11, kutoka katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo na kwenda kuwauza kwa wafugaji.

Aliwataja watu hao kuwa ni Daniel Julius (21), mkazi wa Nsonga na Kamungu Julius (30), mkazi wa Rwimba, ambao walikamatwa na jeshi hilo katika Kijiji cha Mahango, wilayani Mbarali wakiwa wamewauza watoto hao kwa wafugaji.

Kamanda Matei alisema waliku-wa wanauzwa kwa gharama ya Sh. 25,000 na 30,000 na wenye umri kati ya miaka 10 na 14.

Kamanda Matei alisema kati ya watoto 11, wawili walikuwa wameshatambuliwa na kuchukuliwa na wazazi wao na akawataka wananchi kwenda kuwatambua wengine na kuwachukua.

Juzi Nipashe lilipiga kambi katika Kituo cha Polisi Kati jijini Mbeya, ili kujua hatima ya watoto hao na kushuhudia wote waliokuwa wamebakia wakikabidhiwa kwa ndugu zao na Jeshi la Polisi kwa maandishi.

Mmoja wa wazazi wa watoto hao, Kaputila Mwakalobo, mkazi wa Kata ya Swaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema aliridhia mtoto wake kwenda kuchunga mifugo kwa wafugaji wilayani Mbarali, kwa sababu alikuwa mdokozi na amemsababishia hasara.

Alisema waliokuwa wanamhitaji mtoto wake huyo walikubaliana naye kuwa watakuwa wanamlipa mtoto Sh. 100,000 kwa mwaka na mpaka anachukuliwa na polisi alikuwa hajamaliza wiki moja.

"Wakati anaondoka mimi sikuwapo na niliporejea nilikuta ameshaondoka, sikuwa na wasiwasi kwa sababu nilikuwa najua alikokuwa ameenda, ila juzi nikiwa nyumbani nilipigiwa simu kwamba mtoto wangu yupo huku polisi nije nimchukuwe," alisema Mwakalobo. Alisema kutokana na maelezo aliyopewa na Polisi baada ya kumrejesha mtoto huyo, hataruhusu apelekwe tena kwenye shughuli hizo.

Naye Japhet Charles ambaye ni kaka wa mmoja wa watoto hao, alisema mdogo wake baada ya kuhitimu darasa la saba alikuwa hana kazi ya kufanya na waliamua kuridhia apelekwe kuchunga mifugo, ili ajipatie kipato. Alisema familia walikuwa wanajua kuwapeleka watoto kwenda kuajiriwa ni kosa, lakini kutokana na tatizo la kiuchumi waliamua kukubali mdogo wake aende kufanya kazi hiyo.

Alisema alichukuliwa tangu mwaka 2020 na muda wote huo alikuwa anafanya kazi ya kuchunga ng'ombe na wao kama familia waliwahi kwenda kupafahamu alipokuwa anafanya kazi.


**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
**Company No. 22797**

*the bank for your development*

## NOTICE FOR CONVENING AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 2ND OCTOBER 2021 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL FROM 10:00 A.M. (EAT)**

**AGENDA:**
1.0 NOTICE, CONFIRMATION OF QUORUM AND ADOPTION OF THE AGENDA
2.0 TO RECEIVE AND APPROVE THE PROPOSAL FOR ALLOTMENT OF ADDITIONAL SHARES
3.0 CLOSING REMARKS

**NOTE:**

**A. PAPERS FOR THE MEETING**
Papers for the meeting will be available for collection at the Bank's Registered Offices from Monday, 27th September, 2021 and at the meeting venue on the date of the meeting.

**B. OPTION TO JOIN VIRTUALLY**
Shareholders may join the meeting virtually if unable to attend physically, by sending an email to the Company Secretary to register their attendance and obtain meeting access by Monday, 27th September, 2021. The meeting can be accessed virtually only by Shareholders who have registered their attendance in accordance with this notice.

**C. ATTENDANCE BY PROXY**
A Shareholder entitled to attend and vote at this meeting may, if unable to attend in person, appoint a proxy to attend and vote on his/her behalf in accordance with the provisions of the Articles of the Company.

The instrument appointing a proxy must be signed by the respective Shareholder.

The instrument appointing a proxy must be submitted to the Company Secretary at the Bank's registered office or via email by 10.00 a.m. Thursday, 30th September 2021.

**D. TRAVEL AND ACCOMMODATION**
Each Shareholder shall be responsible for the cost of their own travel and accommodation.

**E. OTHER INFORMATION**
Shareholders are reminded to confirm/update their personal information with the Company Secretary.

**F. CONTACT DETAILS FOR COMMUNICATION**

Company Secretary
Akiba Commercial Bank Plc
3rd Floor, Amani Place, Ohio Street
P.O. Box 669
Dar es Salaam

Tel: 0742 972 072 or 0677 152 000
Email: **cs@acbtz.com** or **niwaeli.mziray@acbtz.com**

**By Order of the Board**
Niwaeli Mziray
**Company Secretary**
10th September 2021

**Distribution:**
**Shareholders - Akiba Commercial Bank Plc**

**Invitees:**
**Board of Directors Akiba Commercial Bank Plc**
**Senior Management - Akiba Commercial Bank Plc**
**Director, Banking Supervision Department - Bank of Tanzania**

216451102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Riba mikopo ziangaliwe, elimu iwe kipaumbele

**JUZI** Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, wakati akifungua Kongamano la Wanawake na Biashara jijini humo lililoandaliwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB), alitaka kuwapo kwa ubunifu wa hali ya juu kama nyenzo mahusus ya kuwakomboa wanawake kifedha.

Alisema ubunifu utasaidia kuwafanya kuwa nguvu kubwa ya kiuchumi itakayokuwa chachu muhimu ya maendeleo nchini, na kwamba ni muhimu sana benki nchini zikafanya utafiti kujua ni kwanini wanawake wengi wanashindwa kuchukua na kurejesha mikopo ya benki.

Pamoja na jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia mikopo mbalimbali, bado kuna changamoto nyingi ikiwamo za upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha.

Riba ni kilio cha muda mrefu kwa watu wengi na jitihada mbalimbali zimefanyika, ingawa bado hazijasaidia kupunguza ili kuwezesha watu kupata mikopo kwa ajili ya kuanzisha au kuimarisha biashara zao.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wanawake wamejikuta kwenye mikopo umiza ambayo inatolewa na taasisi binafsi au watu binafsi, kiasi cha kuwa maumivu makali kwa kuwa wanairejesha kwa riba kubwa na kwa muda mrefu kiasi cha kuwa ni mara mbili ya kile kinachostahili kulipwa.

Wanawake wengi wamejikuta wakikimbilia kwenye vikundi vidogo vidogo kama VIKOBA, baada ya kukopa benki, kwa kuwa riba zimakuwa maumivu.

Wito wa Mkuu wa Mkoa Mtaka umekuja kwa wakati sahihi kwamba ni muhimu benki zikaangalia suala hilo, na kuweka utaratibu wa kuwavutia wanawake wengi zaidi kupata mikopo kwa ajili ya kuwekeza, ambako kutakuwa na matokeo kwenye maisha yao binafsi na kuchangia uchumi wa nchi.

Hakuna ubishi kuwa mikopo husaidia kuwawezesha watu kupata fedha za kuanzisha biashara kubwa au uwekezaji mwingine, ambao husaidia kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kuwapo kwa uwezekano mkubwa wa kupata mikopo ya uhakika kunafungua mwanga wa kukua kiuchumi kwa wanawake wengi, lakini ni muhimu kutanguliza elimu ya matumizi sahihi ya mikopo husika ili kuwawezesha kufikia malengo mahususi.

Baadhi ya benki zimeanzisha akaunti mbalimbali za kuyawezesha makundi ya wanawake, watoto na vijana ambazo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kujiwekea akiba, lakini sasa ni muhimu kwa benki hizo kuangalia namna ya kuwa na wanawake wengi wanaokopa na kurejesha mikopo husika.


Tayari tunaona kuna ubunifu wa kuwa na VIKOBA kupitia benki, na baadhi ya vikundi kwa sasa vinaweka fedha benki kutokana na matakwa ya kisheria, lakini bado kuna changamoto nyingi katika kufanikisha hayo.

Pamoja na jitihada za benki, lakini kuna fedha asilimia 10 ya bajeti ya halmashauri inayopaswa kutengwa kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na walemavu kwa ajili ya kuanzisha biashara mbalimbali.

Halmashauri nyingi na hata kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zimeeleza kuwa fedha nyingi zilitolewa, lakini hazikurejeshwa kama ilivyokusudiwa, hali hii inaonyesha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kutoa elimu kabla ya kutoa mikopo.

Tunaamini kwamba elimu kwanza itasaidia kuwawezesha wakopaji kuwa na uelewa kuhusu matumizi ya fedha hizo pamoja na umuhimu wa kuzirejesha kwa wakati mwafaka kuepukana na kujikuta wakifilisiwa mali zao pamoja na athari nyingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Michango mikubwa ya chakula wakati wa mitihani iangaliwe

Na Beatrice Inyasi, TURDACO

**NIWAPONGEZE** wanafunzi darasa la saba wote waliomaliza mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi jana. Ni jambo la heri na hatua katika maisha, wakipumua na kujinasibu ngazi ya umri wa msemo wao wakiwa na msemo 'elowai' wakisubiri kuvuna walichopanda.

Lakini niwakumbushe tu, hapo sio mwisho wa safari ndio kwanza safari myingine, inayonaza kupamba moto. Kadri wanavyosonga mbele katika ulimwengu wa taaluma, ni kugumu na mitihani mingi, hivyo jitihada zaidi zinahitajika. Niwape moyo, penye nia pana njia.

Niseme, kumekuwapo utaratibu kwa shule nyingi za msingi, kila inapofika kipindi cha mitihani ya Taifa, shule huandaa utaratibu wa watoto kupata chakula hapo waliko masomoni.

Kweli dhamira hiyo ni nzuri sana wakitaka wasihangaike, wahusika wanapunguziwa misongamano ya wazazi shuleni kuwaletea chakula.

Pia, kuna sura ya nafuu inayowafanya watoto hao wafanye mitihani pasipo mawazo yenye kitendawili ama chakula kitaletwa au la.

Ingawa jambo hilo ni zuri na liliwekwa kwa nia njema, kwa sasa limekuwa kama msumari wa moto kwa wazazi wengi na hasa wenye uwezo wa chini.

Shule nyingine zimekuwa zikigeuza jambo hilo ni biashara na wala si huduma tena, ambayo watoto wanatakiwa wapatiwe. Ili mtoto aweze kupata chakula, ni lazima alipie.

Ni sawa, kwa sababu shule hazina miradi ya mapishi. Ila malipo yake ndio hapo inapokuwa changamoto. Kwa wastani mtoto anatakiwa kulipa kuanzia Sh. 5,000 mpaka 6,000 kwa siku mbili.

> **Ni sawa, kwa sababu shule hazina miradi ya mapishi. Ila malipo yake ndio hapo inapokuwa changamoto. Kwa wastani mtoto anatakiwa kulipa kuanzia Sh. 5,000 mpaka 6,000 kwa siku mbili.**

Lakini, imefika mbali zaidi kwa baadhi ya shule, kwani watoto hutakiwa kulipa kiasi cha Sh. 10,000 kwa ajili ya mlo wa siku mbili.

Hiyo ni pesa nyingi sana kwa Mtanzania wa kipato cha kawaida ambaye kwa siku hata hiyo 10,000 hawezi kuipata.

Fikiria mzazi ambaye ana watoto wawili na wote wanafanya mtihani. Mzazi huyo atahitajika kulipa kati ya Sh. 10,000 hadi 20,000 kwa siku mbili.

Lakini, kiuhalisia chakula wanachopewa watoto hao ni cha kawaida sana kugharimu kiasi hicho kinachodaiwa.

Watoto wanapewa wali nyama au wali maharage, chakula ambacho kwa kawaida mtaani hakizidi wastani wa Sh. 2,500 tena kwa wafanyabiashara ambao wanahitaji faida.

Hivyo, tunaopata uhalisia kwamba shule zimegeuza mitihani hiyo kigezo cha kupata faida au sehemu ya kujiingiza mapato, huku wazazi wakiumia zaidi kwa upande wao.

Kama Sera ya Elimu inavyoeleza iwe bure kuanzia msingi hadi kidato cha nne, ni vyema mengi yakawa kwa vitendo.

Kama litatokea jambo lolote linalohusu michango, ni vyema shule zikakaa na wazazi na kujadiliana kisha kufikia mwafaka ambao hautawaumiza wazazi kuliko wazazi kuwa watu wa kupokea taarifa na maagizo tu kutoka shuleni. Nashauri ikiwezekana, gharama hizi za chakula katika matukio maalum, ziorodheshwe na ndipo wazazi wakubaliane watalipia kiasi gani kwa kila mtoto.

Hadi sasa serikali inajitahidi sana kuhakikisha, hii sera inafanikiwa. Lakini, kuna baadhi ya walimu hasa shule za msingi wanafanya hiyo sera ionekane ni kama siasa tu.

Tunajua kweli walimu wetu wana nia njema sana na watoto wetu, ila pia muangalie na wazazi walikosimamia msiwaumize katika nafasi yao.

Sio vibaya watoto wakala shuleni, wala sio vibaya wazazi kuchangia, lakini michango hiyo iangaliwe isiwe kwa ajili ya kuwaumiza hawa wazazi wanyonge.

## HABARI KITAIFA




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wapili kushoto), akisikiliza kwa makini maoni na michango mbalimbali iliyotolewa na wadau wa sekta hiyo jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni ni Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji, Tumaini Magesa (wapili kulia) na (kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavuvi wavua risasi 1,400 za SMG ziwani

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAVUVI katika mwambao wa Ziwa Tanganyika wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wamevua viboksi viwili ndani yake vikiwa na risasi 1,489 zinazotumiwa na bunduki aina ya SMG na nyingine za kivita.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, akizungumza na gazeti hili jana kwa simu, alisema wavuvi hao kabla ya viboksi hivyo havijafunguliwa walidhani ndani yake kuna dhahabu.

"Jana (juzi) nilipokea simu asubuhi saa 2:00 kutoka kwa Mzee Jabile kwamba kuna wavuvi ambao amekuwa akishirikiana nao katika utafiti wa madini mwambao mwa Ziwa Tanganyika upande wa kijiji cha Kolongwe, ambao wamepata viboksi viwili na walipokifungua kimojawapo wakakuta ni risasi, hivyo hawakuendelea kufungua cha pili," alisema.

Lijualikali alisema baada ya kupewa taarifa hiyo, yeye na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya walikwenda katika kijiji cha Kolongwe, na walipofika nyumbani kwa Mzee Jabile aliwakabidhi kiboksi kimoja alichokuwa nacho.

Alisema baada ya kukifungua walikuta kuna risasi 739, lakini kiboksi kingine kilichokuwa kimechukuliwa na mvuvi mwingine ambaye alipotakiwa kukileta ili kifunguliwa alikataa akitaka kwanza apewe fedha kwani aliamini kuwa ndani yake kulikuwa na mali (dhahabu).

"Mzee Jabile alitafuta fedha kiasi alichokuwa anakihitaji mvuvi huyo ambapo alimtuma kijana wake ili akakikomboe kiboksi na baada ya kupewa fedha alikitoa," alisema.

Lijualikali alisema kiboksi cha pili baada ya kukifungua kilikutwa na risasi nyingine 750 na hivyo kufanya idadi ya risasi kuwa 1,489 zilizopatikana ndani ya viboksi hivyo.

Alisema baadaye yeye na kamati yake walikwenda hadi mwambao wa Ziwa Tanganyika eneo vilipopatikana viboksi hivyo kufanya uchunguzi zaidi, lakini hakubahatika kupata viboksi vingine zaidi.

"Nimeviachia vyombo vya ulinzi na usalama viendelee kuchunguza suala hili, na kama kuna kosa lolote la kijinai vichukue hatua kali kwa wahusika," alisema.

Kufuatia tukio hilo, Lijualikali ametoa wito kwa wananchi wa Wilaya ya Nkasi waliopo mwambao mwa Ziwa Tanganyika wakiona kitu chochote ambacho sio cha kawaida wasikimbilie kukifungua, badala yake watoe taarifa kwa mamlaka ili wafanye uchunguzi ni kitu gani.

# Maazimio manne bunge kuibana serikali kuhusu ununuzi mahindi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limepitisha maazimio manne ya kuibana serikali kuhusu kusuasua kwa ununuzi wa mahindi, ikiwamo kuitaka kufungua mipaka ya nchi ili wafanyabiashara wauze nje ya nchi.

Hata hivyo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema serikali imesikia kilio chao na itatoa taarifa bungeni leo kuhusu utaratibu utakaotumika kununua mahindi kutoka mikononi mw wakulima.

Jana, Bunge lilitumia takribani saa moja kwa ajili ya wabunge kujadili kusuasua kwa ununuzi huo kufuatia hoja ya dharura iliyowasilishwa na Mbunge wa Kilolo (CCM), Justine Nyamoga. Katika hoja yake, Nyamoga alisema kuna kusuasua kwa ununuzi wa mahindi mwaka huu jambo linalosababisha wakulima kukosa fedha za msimu ujao.

Kutokana na hoja hiyo, Naibu Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, aliruhusu mjadala huo kufanyika kwa saa moja na wabunge kuitaka serikali kununua mahindi yote kwa wakulima huku wengine wakiitaka kufungua mipaka ili wakulima wauze masoko ya nje ya nchi. Akisoma maazimo hayo, Dk.Tulia alisema bunge linaazimia fedha ziongezwe, vituo vya kununulia mahindi viongezwe, mipaka ya nchi ifunguliwe ili wafanyabiashara wauze mahindi nje na bei za pembejeo zishuke kabla ya msimu ujao.

"Tunaamini katika taarifa itakayotolewa na Waziri Mkuu kesho (leo) mambo haya yatapata ufafanuzi. Kwa ujumla bunge limetaka serikali iongeze fedha ili wakulima wauze mahindi yao, vituo viongezwe, mipaka ifunguliwe, bei za pembejeo zipungue bei," alisema.

kabla ya maazimio hayo, Waziri Mkuu Majaliwa alifafanua kuwa serikali ilianza kununua mahindi kupitia Bodi ya Mazao Mchanganyiko takribani mwezi mmoja sasa pamoja na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

"Uzalishaji umekuwa ni mkubwa tumeendelea kuweka utaratibu wa kununua mazao haya, serikali kwanza kununua, lakini kupitia uzalishaji huu tumezungumza na mataifa jirani Kenya, Sudan, Burundi ni kweli nchi hizi zimelima na kuzalisha pia mazao haya,"alisema.

Alisema serikali ilitoa Sh.B ilioni 14 kuipa NFRA na kuagiza kufungua matawi kila Wilaya ili kuwafikia wakulima karibu.

Majaliwa alisema serikali imesikia suala hilo na itatoa taarifa ya kuwapa matumaini wakulima ili waendelee na mikakati yao ya kulima. Kuhusu upatikanaji wa pembejeo, Majaliwa alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa fursa kwa watanzania kuagiza mbolea popote duniani ili kuongeza ushindani utakaopunguza wimbi la bei kubwa ya mbolea.

Pia alisema kiwanda kikubwa cha mbolea kinatarajiwa kujengwa Nala jijini Dodoma kutokana na kupatikana mwekezaji kutoka Burundi.

MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED
"Sisi Kazi tu"

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK** tutauza kwa mnada wa hadhara Nyumba. Minada itafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini, Mnada utafanyika kuanzia saa 4:30 masubuhi na kuendelea.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA.**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | EMILY DANIEL SETEBE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK/YBV/MHB1/34, ILIYOPO YOMBO VITUKA, DAR ES SALAAM. | 2/10/2021 JUMAMOSI |
| 2 | YUSUPH ABDALLAH MCHINJA | i NYUMBA ILIYOPO WAZO-NYAKASANGWE, DAR ES SALAAM<br>ii KIWANJA KIMOJA (1) KILICHOPO KUNDUCHI, TEGETA | 9/10/2021 JUMAMOSI |
| 3 | TITUS D. NYIKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK/MBGL/KGG34/2017, ILIYOPO MBAGALA KINGUGI | 16/10/2021 JUMAMOSI |
| 4 | SK TWIN'S PARKS HOTEL | NYUMBA, KIWANJA NA.36, KITALU "B" ILIYOPO MANGESANI, BAGAMOYO MJINI | 23/10/2021 JUMAMOSI |
| 5 | MAGORI MWITA CHACHA | NYUMBA ILIYOPO KIVULE WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM. | 30/10/2021 JUMAMOSI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14 au ndani ya muda utakaowekwa kwa makubaliano kati ya Bank na Mnunuzi.
2. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4. Dhamana itauzwa "kama ilivyo"

**MKURUGENZI MTENDAJI,
MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD
JENGO LA MWALIMU HOUSE, ILALA BOMA
S L P 62070, DAR ES SALAAM.
SIMU 0755 506970/0716763571**

216451702

# Wafundwa utaratibu uchangiaji wa damu

**Na Richard Makore,** MWANZA

WATANZANIA wametakiwa kuchangia damu kwa kufuata utaratibu badala ya kutoa mara kwa mara bila mpango kuepuka hatari kwa afya ya mtu.

Ushauri huo ulitolewa hivi karibuni na Meneja wa Kanda ya Ziwa wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Dk. Iragi Ngerageza, alipozungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema mwanamume anatakiwa kutoa damu kila baada ya miezi mitatu na mwanamke miezi minne na kwamba kabla ya muda huo, kupita mtu hatakiwa kuchangia damu ili kulinda afya yake.

Dk. Ngerageza alisema damu inatolewa bure kwa maeneo yote ya kutolea huduma za afya, vikiwamo vituo vya afya na hospitali za binafsi na serikali.

Aliongeza kuwa baadhi ya watumishi wa sekta ya afya huamua kukiuka maadili na kuamua kuuza damu kwa ndugu wa wagonjwa.

Kuhusu ukusanyaji wa damu, Dk. Ngeregeza alisema wanatarajia kukusanya uniti 2,630 za damu katika kampeni ya siku nne ya kuchangia damu inayotarajiwa kuanza Septemba 20 hadi Septemba 24, mwaka huu.

Alisema mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unataka kila watu 1,000, watu 10 katika jamii wachangie damu kwa hiari.

Aidha, alisema kwa upande wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama Kanda ya Ziwa wamefikia watu saba kati ya 1,000 wanaochangia damu kwa hiari.

Alibainisha kuwa makundi ya damu yenye vinasaba vya RhD-(negative) upatikanaji wake ni mgumu, ikilinganisha na makundi mengine na kwamba upatikanaji wake haufiki asilimia mbili.

Aidha, alisema kwa sasa wanalenga kukusanya asilimia tatu ya lengo la makusanyo ya kila mwaka na kwamba kwa kituo cha Kanda ya Ziwa mwaka mzima wanalenga kukusanya uniti 20,000.

Alisema makundi ambayo yanashiriki zaidi katika kuchangia damu ni pamoja na wanafunzi wa sekondari, vyuoni pamoja na taasisi za kidini na kwamba unapotokea uhaba wanashirikisha jamii nzima.

"Mwitikio wa jamii katika kuchangia damu bado ni mdogo tofauti na shuleni na wanaofika kituoni kuchangia damu kwa hiari kila siku ni watu watano na mwaka huu tumelenga wafikie watu saba ili kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa damu muda wote," alisema Ngerageza.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Ukusanyaji wa damu cha Kanda ya Ziwa, Hilda Fidelis, alisema kuwa makundi ya watu yanayohitaji zaidi damu ni pamoja na wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, watu wanaopata ajali, wanaofanyiwa upasuaji na watu wenye magonjwa ya kudumu.

# Kukosekana wosia ndicho chanzo migogoro ya familia

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MIGOGORO mingi ya mirathi kwenye familia inaelezwa kutokea kipindi ambacho mzazi mmoja anapofariki na kushindwa kuacha wosia mapema kwenye familia.

Kutokana na hali hiyo Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), imejikita kutoa elimu ya kuhamasisha jamii kuandaa wosia mapema kuepuka usumbufu baadaye.

Akiongea na waandishi wa habari jana mjini hapa, Kaimu Mkurugenzi wa Ulinzi na Haki za Kisheria RITA, Lina Msanga, alisema yapo mashauri ya mirathi yanafika katika ofisi yao ambayo mengi yanatokana na ndugu kutoelewana baada ya kukosekana wosia.

"Tumeona tuhamasishe umuhimu wa wosia tumekuwa tukitoa mafunzo kwa viongozi wa ngazi mbalimbali, hii ya sasa tumeanza kushuka chini kwa wenyeviti wa mitaa na vijiji ambao wapo karibu na wananchi na watafikisha ujumbe kwa haraka," alisema.

Alisema yapo mashauri 104 ambayo wanaendelea kuyashughulikia ili wahusika wapate haki yao.

Alisema kuwa tayari RITA imetoa elimu ya uhamasishaji wa uandishi wa wosia kwa mikoa 10 nchini lengo likiwa kupata mwarobaini wa migogoro ya mirathi kwenye familia.

Akifungua mafunzo kwa wenyeviti hao, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alisema watu wengi hususani wanawake wanakosa haki zao kutokana na kukosekana kwa wosia.


Alitoa wito kwa wananchi kupata ushauri kutoka kwenye taasisi husika kuhusu uandishi wa wosia ambao utaondoa migogoro ya mara kwa mara kwa jamii.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Galagaza, Wilaya ya Kibaha, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kwenda kukabiliana na kesi walizokuwa wakizipokea mara kwa mara kutoka kwa wananchi wao ambayo inasababishwa na kugombea mirathi ya marehemu.

Subira Kindula, Mtendaji Kata, Boko Mnemela, alisema wosia una umuhimu kwenye familia kwa kuwa utamsaidia mwanafamilia kupata haki bila kuwapo kwa migogoro baada ya mmiliki wa mali kufariki.

Akitoa mada ya wosia, Janeth Mandawa, kutoka RITA aliwataka wananchi kuachana na mila potofu ya kuwa ukiandika wosia mapema ni kuharakisha vifo.

Janeth alisema dhana hiyo inatakiwa kupingwa na viongozi kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kuwa tangu 2008 RITA wamepokea wosia 810 na kati ya hizo 57 pekee ndiyo wamechukua nakala baada ya mtoa wosia kufariki.



Mtaalamu wa bia za mitungi wa TBL, Hashim Sarakikya, akionyesha mashine za kuuzia bia kwa ujumbe wa wakala wa kusambaza bia za mitungi kutoka Zanzibar, walipofanya ziara ya kikazi katika Kiwanda cha TBL Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walalamika ucheleweshaji malipo TBA

**Na Richard Makore,** MWANZA

UCHELEWESHWAJI wa malipo katika miradi mbalimbali inayofanywa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Mkoa wa Mwanza inakwamisha miradi hiyo kukamilika kwa wakati.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Meneja TBA, Mkoa wa Mwanza, Moses Urio, alipozungumza na Nipashe.

Alisema wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali wakati mwingine inachukua miezi sita baada ya kuwasilisha hati za malipo kwa mshitiri (client) kupata malipo ya mradi.

Alisema hatua hiyo inasababisha taasisi yenyewe kutafuta ufumbuzi kwa kutumia gharama zake kwa muda ambao hawajapata malipo ama kusimamisha ujenzi kwa muda.

Aidha, alisema wanakabiliwa upungufu wa upatikanaji wa vifaa kwa wakati kutokana na kuwapo kwa miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa katika Mkoa wa Mwanza.

"Kutokana na miradi mikubwa inayoendelea katika mkoa huu kuna uhaba wa upatikanaji wa vifaa kama vile kokoto na nondo, kwa kuwa maeneo yanayozalisha malighafi hizo ni yaleyale na uhitaji umeongezeka kwa sababu ya miradi kuwa mingi," alisema Urio.

Kadhalika, alisema wajibu wao ni kuhakikisha wanasimamia miradi yote wanayotekeleza kukidhi ubora unaotakiwa kwa kutumia wataalam waliosemea masuala ya ujenzi na kuhakikisha ujenzi huo unafanyika kwa gharama nafuu. Alisema miradi yote ambayo imekamilika wametekeleza kwa ubora ikiwamo mradi wa ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Ofisi ya Nyaraka za Taifa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana.

Akizungumzia upangishaji wa nyumba wanazomiliki alisema wanakumbana na adha ya wapangaji kutolipa kwa wakati, kurithishana nyumba pamoja na wapangaji kutotunza mazingira ya ndani na nje ya nyumba hizo kama mikataba inavyowataka.

Alisema malengo yao ya upangishaji ni kwa ajili ya watumishi wa serikali na wanatoa nafasi kwa watu binafsi pia lakini kodi inakuwa tofauti.

"Mtumishi anapopanga nyumba zetu thamani ya kodi ni 2/3 kulingana na soko na kwa watu binafsi wanalipa kodi ya kawaida kulingana na soko," alisema Urio.

Alitoa wito kwa watumishi wao kufanya malipo ya miradi inayotekelezwa kwa wakati kwa lengo la kukamilisha miradi hiyo kwa muda husika.

## W'biashara wapata mwamko kuthibitisha ubora wa bidhaa zao

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WAFANYABIASHARA na wajasiriamali mkoani Lindi wamepata mwamko wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao pamoja na kusajili majengo ya chakula na vipodozi kupitia elimu ambayo imetolewa na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuanzia Agosti 31, hadi Septemba 6, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Lindi kuhusiana na majumuisha ya kazi ambayo maofisa wa shirika hilo wamefanya katika wilaya tatu za mkoa huo, Ofisa Usalama wa Chakula wa TBS, Barnabas Jacob, alisema wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu wamefikia walengwa wengi.

"Tumeweza kufikia welengwa wengi tuliokuwa tukiwatarajia katika wilaya za Liwale, Nachingwea na Lindi na wameahidi kujitokeza kuthibitisha ubora wa bidhaa zao pamoja na kusajili majengo ya chakula na vipodozi ili waweze kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria," alisema Jacob.

Jacob alisema katika wilaya hizo wamefanya ukaguzi kwenye maduka ya vyakula na vipodozi, kutembelea wajasiriamali wadogo wanaofanya uzalishaji wa bidhaa ili kuwahamasisha kupata alama ya ubora.

Alisema katika Wilaya ya Lindi wajasiriamali 18 wameahidi kuanza mchakato wa kuthibitisha ubora wao.

Alisema wilayani Lindi wametoa elimu kwa umma kwa watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) kuhusu madhara ya matumizi ya bidhaa hafifu, hususani vipodozi ambavyo vimekatazwa kutumika nchini kutokana na kuwa na viambata sumu vyenye madhara kwa afya za watumiaji.

Kwa upande wa Wilaya ya Nachingwea watumishi waliopatiwa elimu hiyo ni wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), TRA, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), TTCL na wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Jacob alifafanua kwamba elimu hiyo itawawezesha watumishi hao kuwa mabalozi wazuri ndani ya jamii na familia zao kwa ujumla.

Alisema elimu hii imelenga taasisi za umma ikiwa ni mwendelezo wa shirika kutoa elimu kwa umma kuhusiana na madhara ya vipodozi na vyakula vilivyopigwa marufuku," alisema Jacob na kuongeza;

"Watumishi katika taasisi ambazo tumetoa elimu wamepata mwamko mkubwa na wametuahidi kuwa mabalozi kwa watu wengine ikiwamo familia na jumuiya zinazowazunguka kuhusiana na madhara ya vipodozi hivyo," alisema Jacob.

Kama ilivyo kuwa kwa Wilaya ya Lindi, Jacob alisema na Nachingwea walitembelea viwanda ambavyo vimethibitishwa na TBS ili kuangalia kama vinaendelea kuzalisha bidhaa kwa mujibu wa viwango walivyopewa.

Kwa upande wa Liwale, Jacob alisema mbali na kutoa elimu kwa wajasiriamali na wafanyabiashara, walifanya ukaguzi wa awali kwa wenye viwanda ambavyo wazalishaji wake wanataka kupata alama ya ubora.

Alitaja miongoni mwa viwanda ambavyo maofisa hao wa TBS wamefanya ukaguzi na kuhamasisha kujitokeza kupata alama ya ubora kuwa ni pamoja na vile vinavyokamua mafuta ya alizeti, viwanda vya kubangua korosho, kwenye mashine za kusaga unga pamoja na kiwanda cha uzalishaji wa bidhaa za mikate.

# Wanawake wakwazwa kupata ajira kwenye sekta ya uziduaji

**Na Yasmine Protace**

WADAU wa Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), wamesema kuwa masuala ya usawa wa kijinsia yamekuwa yakiikumba sekta ya uziduaji, ambapo hali hiyo inasababisha wanawake kukumbana na kikwazo katika kupata ajira katika sekta hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ni wanawake wachache wanaopata ajira katika sekta ya uziduaji ambayo inajumuisha masuala ya uchimbaji wa madini, mafuta na gesi.

Imeelezwa kuwa nafasi nyingi kwenye sekta ya uziduaji zinashikiliwa na wanaume.

Hayo yalisemwa na Hassan Juma, mmoja wa washiriki katika semina za GDSS ambazo huratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"Ukiangalia katika sekta ya uziduaji, wanawake wanakuwa wachache, hivyo hali hiyo inaweza ikasababishwa na wanawake kutoweka mkazo katika kusoma masomo ya sayansi," alisema.

Aliongeza kuwa inatakiwa wanawake wajiunge kwa wingi katika masomo ya sayansi, na kwamba hali hiyo, itachangia kuwapo kwa idadi ya wanawake wengi.

Shakila Malumana, mfanyakazi wa TGNP Mtandao, ndiye aliyebainisha hayo alipokuwa akitoa mada inayohusu TEIT MSG na sekretarieti .

"TEIT MSG na Sekretarieti maana yake ni taasisi ya uhamasishaji na uwajibikaji, uwazi katika sekta ya madini na gesi," alisema.

Aliongeza kuwa kuna asasi ambazo zinafanya kazi ya utafiti na serikali kupitia TEIT MSG Sekretarieti.

Joseph Mapunjo, alisema kutokana na taasisi hiyo kusimamia masuala ya uziduaji, kuna haja hatua kali zichukuliwe kwa wale wanaochimba michanga na kushindwa kuyafukia mashimo yao.

Akizungumzia masuala ya uziduaji katika mlengo wa kijinsia, alisema kuwa kuna haja elimu kwa jamii iendelee kutolewa ili kuleta usawa katika kazi kwa pande zote mbili.

" Wapo wanawake waliosoma na wana uwezo wa kufanya na wakaleta maendeleo," alisema.

Monica John, Ofisa wa TGNP Mtandao, alisema kuna haja ya elimu kutolewa kuhusu TEIT ambayo itasaidia kujua kazi zinazofanywa na TEIT.



Wajumbe wa Serikali ya Kijiji cha Kakisheri, Kata ya Nyakatende, Musoma Vijijini mkoani Mara, Benjamin Lazaro (kushoto) na Majira Makoba, wakipanga viroba vya mchanga unaosombwa na wananchi wa kijiji hicho kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu kwa Shule ya Msingi Kambarage ya kijijini hapo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva, wamachinga Mabibo waondolewa hofu

**Na Paulina Chimeledya,** TUDARCo

MADEREVA na wafanyabiashara wa Mabibo Sokoni Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam wametakiwa kuwa wavumilivu kutokana na usumbufu wanaoupata katika uboreshaji wa barabara ya Mabibo Sokoni kutoka Urafiki mpaka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

Ushauri huo ulitolewa na Mratibu Msaidizi wa Mradi wa ujenzi wa miundombinu (DMDP) Manispaa ya Kinondoni, Mkelewe Tungaraza, ambaye ndiyo msimamizi wa ujenzi wa kipande hiko cha barabara kutoka Urafiki hadi NIT, ambapo ameeleza kuwa kwa sasa utekelezaji unaendelea na kufikia asilimia 65, hivyo wananchi, wafanyabiashara na madereva usumbufu wanaoupata ni wa muda mfupi.

Pia alieleza namna ambavyo wafanyabiashara watanufaika kutokana na ujenzi huo ambapo watalifanya eneo kuwa la kibiashara zaidi kwa kujenga miferеji, eneo la kuegeshea magari, kwa ajili ya wanunuzi pamoja na kuwekewa taa za sola zitakazowapa fursa wafanyabiashara ya kufanya biashara wakati wowote huku akisisitiza ulinzi wa miundombinu hiyo.

"Na niwatoe wasiwasi wafanyabiashara wa eneo la Mabibo Sokoni na maeneo mengine kuwa ni muda wao sasa wa kufanya biashara hadi usiku kwani kipande hicho kitawekwa taa ambazo zitakuwa zinawaka usiku mzima... kwa hiyo watakuwaa watafanya biashara zao hadi usiku ikiwapendeza" alisema Mkelewe Tungaraza.

Aidha, amewatoa wasiwasi wafanyabiashara na watumiaji wa barabara hiyo kuwa ipo katika hadhi ya barabara ya mtaa, lakini hata hivyo wamezingatia umuhimu wa barabara hiyo na itakuwa yenye kiwango bora cha kuruhusu magari zaidi ya tani kumi.

Wafanyabiashara wadogo wanaofanya shughuli zao kando ya barabara hiyo, walieleza kufurahishwa na uboreshaji wa miundombinu ya barabara hiyo na kuwa na mwangaza wa kutosha kuwarahisisha shughuli zao.

Kwa upande wa wafanyabiashara wadogo wanaofanya shughuli zao kando ya barabara hiyo, walieleza kufurahishwa na mwenendo wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara hiyo kutokana na kuwa na mwangaza mkubwa kuwarahisishia shughuli zao hasa kutokana na kujengwa kwa haraka, ingawa wakati mwingine bado wateja wao wanaghalamika kuzunguka barabara za ndani ndani kusaka huduma.

"Takribani mwezi mmoja mpaka sasa tumekuwa tukipisha ujenzi huu, lakini sasa tunanufaika...ni mwezi tu, lakini tunaona hata lami inakaribia kuwekwa, hivyo tunafurahi kwa maendelea haya na tunaimani ukikamilika tutanufaika ziadi hasa kwenye suala la usafirishaji was bidhaa zetu," alisema Ezekiel Muna, mfanyabiashara Soko la Mabibo.

Hadi sasa kipande hicho cha barabara kimekamilika kwa asilimia 65 na hadi kufika mwishoni mwa mwezi huu, kipande hicho cha barabara kitakuwa kimemalizika na kuendelea kutumiwa na magari na kuepusha adha ya usafiri.

# Utafiti wa mamba kwenye mito mikoa mitatu waendelea



Habari zote na Augusta Njoji

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inaendelea kufanya tathmini ya mamba katika mito iliyopo mikoa ya Katavi, Rukwa na Morogoro.

Wizara ya Maliasili na Utalii iliyasema hayo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Morogoro Kusini (CCM), Innocent Kalogeris.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani kuvuna mamba katika Mto Ruvu hasa katika Vijiji vya Kigamila, Bwila Juu, Magogoni, Bwila Chini, Kongwa, Tulo, Lukuhinge, Kata za Mvuha na Serembala katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini ili kupunguza vifo vinavyosababishwa na mamba hao na kuondoa adha kwa wananchi hao.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema baada ya tathmini hiyo kukamilika na kubainika kuwa idadi ya mamba waliopo ni kubwa, mamba hao watavunwa.

Aidha, ilisema endapo itabainika kuwa idadi ya mamba katika maeneo husika ni ndogo, serikali itabaini mamba wanaosababisha adha kwa wananchi na kuwavuna ili wasiendelee kuleta madhara kwa wananchi.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, Christopher Ole Sendeka (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa Viti Maalumu, Neema Lugangira (kulia), Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ashauri kuwabana zaidi wanaotapeli, wizi wa mitandaoni

MBUNGE wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, ameitaka serikali kuweka mikakati ya ziada ya kudhibiti tatizo la utapeli na wizi wa kimtandao kupitia simu za mkononi.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji serikali ina mikakati gani ya ziada katika kulikabili suala hilo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, serikali tayari imechukua hatua za kuweka mazingira salama kwa wananchi hususan kwenye mitandao.

Ilitaja hatua hizo ni mwaka 2015 serikali ilitunga Sheria ya Makosa ya Mitandao kwa lengo la kutambua kisheria makosa yanayofanyika kwenye mitandao ili kuweza kuchukua hatua stahiki yanapobainika makosa hayo.

Pia ilisema Sheria ya Miamala ya Kielektroniki kwa lengo la kutambua miamala inayofanyika kimtandao.

Aidha, ilisema hatua nyingine ni serikali ilianzisha Kitengo cha Uhalifu wa Mitandao chini ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa ya mitandao ikiwamo wizi wa aina yoyote kwenye mtandao na kuandaa majalada ya kufungulia mashtaka kwa kusaidiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Ilisema watuhumiwa wanaokamatwa kutokana na matumizi mabaya ya mitandao huchukuliwa hatua stahiki.

Hata hivyo, ilisema Februari 2021 serikali imeunda Kamati ya Taifa ya kusimamia utatuzi wa matumizi mabaya ya huduma na bidhaa za mawasiliano ambayo inahusisha wizara na taasisi zote zinazohusika katika kushughulikia makosa ya mtandao.

Ilisema kamati hiyo ni kamati ya kudumu na inaishauri serikali namna ya kutatua kero za mitandao.

Ilifafanua kuwa serikali kwa kushirikiana na watoa huduma wa simu za mkononi imeanzisha mfumo kupitia namba '15040' wa kupokea na kuzifungia namba ambazo zimeripotiwa na kuthibitika kutuma ujumbe au kupiga simu za utapeli.

Ilisema baada ya kuthibitisha namba hizo kufanya vitendo hivyo, namba husika hufungiwa, kitambulisho cha NIDA kilichotumiwa kusajili namba husika kufungiwa kusajili na kifaa kilichotumika (simu) pia kufungiwa ili kisifanye kazi.

Aidha, ilisema serikali itaendelea kuongeza jitihada za kuelimisha umma matumizi mazuri na sahihi ya TEHAMA kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

# Sekondari 1,000 za kata kujengwa

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imejipanga kujenga shule za sekondari za wasichana kila mkoa na nyingine 1,000 kwa kata zisizo na shule hizo.

Hatua hiyo inalenga kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na vikwazo hususani watoto wa kike kutembea umbali mrefu.

Ofisi hiyo ilibainisha hayo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itajenga Shule ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Sita Mungaa ambayo ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa kipindi cha kampeni 2020 alipopita kwenye jimbo hilo.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema shule 26 za wasichana zitajengwa kwa kila mkoa.

Vile vile, alisema serikali itafanya upanuzi wa shule za sekondari 100, ili kupokea wanafunzi zaidi wa kidato cha tano na sita.

Ilisema ujenzi wa shule zote mpya za sekondari na upanuzi wa sekondari za kidato cha tano utafanyika kwa awamu.

Ilibainisha awamu ya kwanza ya ujenzi itaanza mwaka wa fedha 2021/22 ambapo serikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 220.

Ilisema kabla ya kuanza ujenzi, serikali itafanya tathmini ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya na mahitaji ya upanuzi wa sekondari za kidato cha tano na sita ikiwa ni pamoja na Shule ya Sekondari Mungaa.

# Uboreshaji wa maombi miradi kimkakati h'shauri

SERIKALI imesema inaangalia njia bora itakayosaidia kuboresha utaratibu wa maombi na vigezo vya uandaaji wa miradi ya kimkakati kwa halmashauri kabla ya utoaji wa fedha.

Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa kauli hiyo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuhuisha vigezo vya mfumo wa miradi ya kimkakati kupitia maandiko ya miradi ili kusaidia halmashauri kubuni miradi ya kiuchumi.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, imejikita katika kutoa huduma bora na zenye uhakika kwa wananchi wake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendelea kujiongezea mapato kwa kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao ili kutoa huduma bora kwa lengo la kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Ilisema ili kufikia lengo hilo serikali iliandaa mkakati maalum wa kuziwezesha halmashauri kujitegemea kimapato.

Ilibainisha kuwa katika kutekeleza mkakati huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha zinatumia kwa ukamilifu fursa za kimapato zilizopo katika maeneo yao na kuongeza uwezo wa kujitegemea kimapato.

Ilisema fedha za kugharamia miradi mkakati hutolewa kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na wizara.



Ukurasa 12

Madereva Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli walalama hatari ya corona kwa wateja abiria




Ukurasa 13

Wabongo propaganda zetu zitatuponza!



Ukurasa 14

Zanzibar inavyoibuka upya kinara mzalishaji, muuzaji viungo duniani

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 10, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Kusini nao wamejitosa rasmi kuwa mzalishaji mafuta kula

**Na Sabato Kasika**

MAHITAJI ya mafuta ya kula nchini ni tani 570,000, lakini yanayozalishwa ni tani 250,000 pekee. Pengo la mahitaji linaagizwa njwe ya nchi.

Wizara ya Viwanda na Biashara, inasema kuna tani 365,000 zinazoagizwa nje, ili kukidhi mahitaji. Ni hali inayoonyesha haja ya kuwekeza zaidi kwenye kilimo cha mafuta ya kula kama alizeti, ufuta, mawese, karanga na pamba, ili kuongeza uzalishaji na ziada ya kuuzwa nje.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dk. Geoffrey Mkamilo, anawataka wakulima waongeze uzalishaji wa mazao hayo, ili kuokoa pengo la Sh. milioni 443 zinazotumika kuagiza mafuta hayo ughaibuni.

Anawaambia wakulima wa ufuta wilayani Nachingwea mkoani Lindi, alipotembelea shamba darasa la ufuta katika Kijiji cha Mkumba, anasema ni hali inayoifanya TARI kuweka mkakati wa kuhakikisha uzalishaji mafuta unapanuka.

Mipango hiyo ni pamoja na kutoa elimu sahihi kwa wakulima wazalishe kwa tija mazao ya mafuta kama michikichi, alizeti, ufuta, karanga na pamba.

"Nimetembelea Kijiji cha Mkumba Wilaya ya Nachingwea Mkoa wa Lindi, ili kuhamasisha wakulima walime zaidi na tunatarajia kuzalisha zaidi ya tani 35,000 za mbegu, kwa ajili ya kilimo cha ufuta," anasema Dk. Mkamilo.

Anafafanua kwamba mkoani Kigoma, TARI imetoa mbegu za michikichi zinazozalisha mafuta mengi, pia alizeti mkoani Singida na Dodoma, wakiwahimiza kilimo zaidi.



Hassan Mpako, akiwa katika shamba lake la alizeti. **PICHA: SABATO KASIKA**

### WADAU WAUNGA MKONO

Wakati TARI ina mikakati kuimarisha kilimo cha mazao ya mafuta, wadau wa kilimo wilayani Liwale, mkoani Lindi, wameanzisha taasisi ya kuhamasisha kilimo cha alizeti wilayani humo.

Taasisi hiyo, Liwale Social Economic Development Organization (LSD-Organization), waasisi wake ni viongozi waliohudumu katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Ruangwa, Nachingwea na Liwale (RUNALI).

Mwenyekiti mstaafu wa RUNALI, Hassan Mpako, anaiambia Nipashe, kwamba pamoja na waasisi wenzake; Hashimu Majangagara, Ally Kamuna na Said Mulila, wanahamasisha ulimaji alizeti, Liwale. Anasema, hapo wanaweza kuwageuza wakulima waache mazoea ya kutegemea korosho, ufuta na mbaazi kama mazao pekee ya biashara.

Mpako anasema, tofauti na korosho inayochukua miaka mitatu kufikia hatia ya mavuno tangu kupandwa, kilimo cha alizeti kinachukua kati ya miezi mitatu hadi minne kuanzia upandaji hadi mavuno.

"Vilevile kilimo cha alizeti kina faida kubwa, kwani mafuta yake yanahitajika kwa wingi, ndani na nje ya nchi, na mashudu yake ni chakula cha mifugo, hivyo ni vyema kuhamasisha wakulima wachangamkie fursa hii," anasema, huku akikiri wakulima hawajachangamkia .

### UHAMASISHAJI UTAKAVYOKUWA

Mpaka, ambaye kwa sasa ni ni Mkurugenzi wa Uhamasishaji wa asasi LSD-Organization, anataja matarajio yaliyopo ni kuanza uhamasishaji kilimo hicho, mara tu baada ya kuzinduliwa rasmi siku tano zijazo, yaani Septemba 15.

"Kwa sasa tuko kwenye maandalizi ya uzinduzi na tumedhamiria kusaidia wakulima kubadilika na kuacha mazoea ya muda mrefu ya kutegemea korosho, ufuta na mbaazi kama mazao ya biashara, badala yake waongeze alizeti," anasema.

Anafafanua kazi ya kuhamasisha kilimo cha zao, wanataka wawapate wakulima 2,000, ambao kila mmoja atakuwa na ekari moja ya alizeti na taasisi yao itawagawia mbegu na viuatilifu.

"Kwa kawaida, ekari moja hutoa kilo 500 za alizeti. Taasisi yetu ikiwa na wakulima 2,000, wanaweza kupata tani 1,000,000 za alizeti, ambazo makisio ya chini ni kutoa lita 400,000 za mafuta," anasema.

Mpako anafafanua, asasi yao inadhamiria kumiliki mitambo ya kukamua mafuta ya alizeti na mwingine wa kuchakata mashudu ya chakula cha mifugo.

"Baada ya mavuno ya zao hilo ambayo yatakuwa mwanzoni mwa mwaka ujao, tutashawishi wakulima hao 2,000, ili wachange fedha zitakazotokana na mavuno ya zao hilo, ili kununua mitambo hiyo," anasema.

"Ninatamani Liwale iwe mfano kwa wilaya nyingine za Mkoa wa Lindi katika kilimo cha alizeti, ili ikiwezekana, wakulima kutoka kwingine wafike wilayani kwetu kujifunza uzalishaji wake," anasema.

### MATARAJIO YAO

Mwenyekiti wa taasisi hiyo wazalisha mafuta, Hashim Majanjagara, anadokeza malengo yao hadi mwanzoni mwa mwaka ujao, sawa na robo mwaka wanatarajia matokeo chanya katika ulimaji mafuta Liwale.

"Wataalamu wa kilimo wanasema kuwa alizeti inaweza kustawi kwa wingi hata huku kwetu mikoa ya Kusini.Nasi tunaona ipo haja ya kuhamasisha wakulima kuongeza zao lingine la biashara badala ya korosho, ufuta, mbaazi," anasema.

Nchini, alizeti inalimwa kwa wingi katika Mikoa Singida, Rukwa, Mbeya, Iringa, Dodoma, Ruvuma na Manyara.

BIASHARA

# Madereva Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli walalama hatari ya corona kwa wateja abiria

- Kupuuzwa huduma; elimu duni; wataalamu wachache
- Uongozi kituo, wasafiri na wasafirishaji, trafiki wanena

**Na Mary Geofrey**



Shughuli zikiendelea katika Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

HADI sasa kuna wastani wa mabasi kati ya 600 na 1,200 huingia na kutoka katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi Ubungo, kila siku hubeba abiria 27,000 hadi 56,000 wanaoingia na kutoka ndani na nje ya nchi.

Kwa maana hiyo, zaidi ya watu milioni 9.8 hadi milioni 20.4 husafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine ndani na nje ya nchi kwa mwaka.

Idadi ya mabasi huongezeka kulingana na msimu. Siku za kawaida kunakuwapo abiria 600 hadi 800 na msimu wa sikukuu hufika kati ya mabasi 800 na 1,200.

Idadi hiyo ya wanaoingia na kutoka mkoani Dar es Salaam, inabadilika kila siku, ila idadi ya madereva ni ileile.

Kwa kutambua umuhimu wa kundi la madereva katika kipindi cha mapambano, dhidi ya UVIKO-19, gazeti la Nipashe kwa kushirikiana na asasi 'Chimbua Communication' mapambano dhidi ya UVIKO -19, ilidodosa uhalisia uliopo.

### MADEREVA MABASI

Katibu Mkuu wa Chama cha Madereva wa Mabasi Makubwa (CHAMAWATA), Abdallah Lubala, anasema hakuna taasisi iliyokwishawapa elimu ya kukabiliana na UVIKO-19 hasa kwa kuzingatia umuhimu wa jukumu lao la kusafirisha abiria, baadhi yao wakiwa wagonjwa.

"Siyo wamiliki wa mabasi wala Wizara ya Afya waliokuja kutupa elimu ya namna ya kuchukua tahadhari, dhidi ya UVIKO-19, badala yake tunachukua tahadhari wenyewe kupitia elimu inayotolewa kwa vyombo vya habari," anasema Lubala.

Anaeleza haja na umuhimu wa elimu ya tahadhari na namna ya kujikinga kwa ukubwa wa majukumu yao kusafirisha watu kutoka ndani na nje ya nchi.

"Tunasafirisha watu kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine. Kila siku tunabadilisha abiria, lakini hatujaona kama serikali imechukulia kundi hili kwa umuhimu na ukubwa huu," anasema Lubada.

Dereva wa mabasi kati ya Dar es Saalam na Morogoro, Juma Isihaka, anasema wamekuwa wakiishi kwa kutimiza majukumu yao ya kazi na siyo kuangalia usalama wao.

"Tajiri anataka usafirishe abiria na siyo kusema kuna UVIKO-19. Tunaweza kupata maambukizi, hili halimhusu bosi na ndio maana madereva tunaendelea na kazi bila kujali chochote," anasema Isihaka.

> **Kila mwananchi akichukua tahadhari binafsi, ni rahisi katika utekelezaji wa tahadhari zinazotolewa katika maeneo ya mkusanyiko.**

Anafafanua kwamba wamekuwa wakisafiri kila siku kuangukia hata kubeba wenye maambukizi, ingawa wanakiri hawajawahi kuzidiwa. Anabakiwa na kiulizo endapo watazidiwa, kwani hawana suluhisho la mara moja.

"Ina maana leo akitokea mgonjwa, anaweza kuambukiza wote bila sisi kujua na kama tukijua ni UVIKO-19, tunaweza tukamtelekeza ndani ya basi, kwa sababu hatuna tunachofahamu," anasema Isihaka.

Dereva Goodluck John, anayeunganisha safari kati ya Dar es Salaam na Songea, anasema wanahitaji zaidi elimu ya kinga na namna ya kuchukua tahadhari, endapo watapata mgonjwa ndani ya basi.

"Tunafanya safari za mbali, mtu anaweza kuzidiwa ndani ya basi tunafanyaje? Hatujui ila kuna haja ya serikali kutambua umuhimu wetu, ili kusaidia kujikinga na maambukizi zaidi ya UVIKO-19," anasisitiza.

### WANAOTETEA ABIRIA

Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), Hassan Mchanjama, anasema katika sekta ya usafirishaji bado elimu inahitajika, kwa kuwa hakuna hakuna tahadhari sahihi na za kutosha zinazochukuliwa.

Anasema wamiliki mabasi hawajafuata mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, unaotaka kuwekwa vitakasa mikono katika mabasi na madereva, huku wanakosa elimu ya kutosha kuhusu uchukuaji tahadhari na kuwahimiza abiria kuvaa barakoa.

"Bado elimu inahitajika katika mapambano ya UVIKO-19 katika sekta ya usafirishaji. Madereva hawana elimu ya kutosha hasa ukizingatia wapo katika hatari kubwa ya maambukizi, kwa sababu wanasafirisha abiria kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine," anasema Mchanjama.

Anasema, tayari wameshaanza mchakato wa kutaka kusaidia utoaji elimu kwa madereva na wasafiri, wakishirikiana na wataalamu wa afya.

"Tumeiomba serikali kutenga fungu kwa kundi hili muhimu, ambalo bado halijatambuliwa kwa umuhimu mkubwa, tupatiwe rasilimali fedha, watu na vitendea kazi katika mapambano haya ya UVIKO-19," anasema Mchanjama.

### TABOA WANENA

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustafa Mwalongo, anasema elimu ya UVIKO-19 bado inahitajika kwa madereva wa mabasi.

Anasema, kuna madereva, ambao waendapo nje ya nchi, wanakuwa hawajapewa elimu hivyo na ni muhimu, suala hilo la elimu likawa endelevu kwa madereva.

Rai ya Mwalongo, ni kwamba serikali iendelee kuongeza nguvu katika vituo vidogo njiani, ambako abiria wanapandia mabasi na hakuna tahadhari zinazochukuliwa.

Anasema hivi sasa, TABOA wanashirikiana na serikali za Manispaa kuhakikisha elimu inatolewa, pamoja na vifaa vya kujikinga, ili kudhibiti maambukizi mapya.

"Tumeanza kuweka vitakasa mikono kwenye mabasi yote katika Kituo Kikuu cha Mabasi Mbezi, ndoo za maji katika milango mitatu ya stendi hii na tunaendelea katika vituo vingine," anasema Mwalongo.

### USALAMA BARABARANI

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilboard Mutafungwa, anaiambia Nipashe kuwapo umuhimu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, kushirikiana nao kutoa elimu zaidi kwa madereva kujikinga na UVIKO-19.

Anasema, kitaifa wamekuwa wakitoa elimu ya kujikinga na UVIKO-19 kwa madereva katika vituo vya mabasi nchini kabla ya kuanza safari, kwa wakishirikiana na wadau mbalimbali nchini.

Kamanda Mutafungwa anaorodhesha jitihada wanazofanya inaujumuisha elimu kwa madereva, kujikinga na kuhimiza abiria kujikinga, sambamba na kuwa na sanduku la huduma ya kwanza, kusaidia dharura ndani ya basi.

Anasema, pia wanawahimiza madereva kujiepusha na ajali za barabarani na ikitokea abiria amezidiwa, anapaswa kupelekwa katika kituo cha afya kilicho jirani.

### HALI HALISI

Nipashe ilipokuwa katika katika Kituo Kikuu cha Magufuli, haikushuhudia hatua madhubuti za tahadhari za kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19.

Sababu za abiria kupuuza na kukiuka kanuni hizo za usalama ni uharaka wa kuwahi mabasi kutoka kituoni, hata wanashindwa kuzingatia tahadhari tajwa.

Abiria Sophia Joseph anasema, watu hawachukui tahadhari, kwa sababu kuna ugumu katika kudhibiti mwingiliano wa watu wengi.

Mwingine, Nora Kamili, anafafanua kukosekana tahadhari madhubuti katika vituo vya njiani, ambako mabasi hayo yanapakia abiria.

Ashura Kilengawana, mkazi wa Mpanda anashauri serikali kuendeleza jitihada za wananchi kujikinga na kuchukua tahadhari kuanzia ngazi ya familia, hasa katika maeneo ya pembezoni.

"Kila mwananchi akichukua tahadhari binafsi, ni rahisi katika utekelezaji wa tahadhari zinazotolewa katika maeneo ya mkusanyiko," anasema Ashura.

### UONGOZI KITUO

Meneja Uhusiano na Ufuatiliaji wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Maira Mkama, anasema Manispaa ya Ubungo peke yake ndio imetoa wataalamu wake kutoa elimu ya kujikinga na UVIKO-19, kwa watumiaji wote wa kituo hicho.

"Bado tunahitaji elimu zaidi kwa madereva wetu, ambao wanasafiri kutoka na kuingia kila siku katika kituo hiki kutoka kwa wataalamu wengine wa Wizara ya Afya," anasema.

Anafafanua kuwa, Manispaa pia imepeleka huduma ya chanjo katika kituo hicho katika kudhibiti kuenea kwa UVIKO-19.

Kuhusu vifaa vya kujikinga, anasema wamepokea msaada wa vitakasa mikono na kuvifunga katika mabasi yote na vifaa vya kunawa mikono katika milango ya kuingia kituoni hapo.

### MWONGOZO WIZARANI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Abel Makubi, ilitoa mwongozo wa kupunguza misongamano katika maeneo mbalimbali nchini, hasa katika vituo vya mabasi na abiria wanaosafiri kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19.

Vyombo vya usafiri imeshauriwa kuwa wasafiri wawezeshwe kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kabla ya kupanda, viongozi wa mtaa husika wahakikishe kuna vyombo vya kuhifadhia maji na sabuni ya kutosha katika kila kituo.

Aidha, uongozi wa vituo vya mabasi unatakiwa kusimamia vifaa vya kunawa kwa maji tiririka na kuhakikisha abiria wote wananawa mikono.

Jambo la pili, Makubi anawashauri wamiliki wa vyombo vya usafiri kuhakikisha wanaweka vitakasa mikono katika vyombo vya usafiri, huku kila anayeinga atimize sharti la kuvaa barakoa, kama ilivyoelekezwa kwenye mwongozo, isipokuwa watoto wenye umri chini ya miaka minane.

Lingine anataja haja ya utoaji elimu ya umuhimu wa kutosongamana ndani katika vituo vya mabasi kupitia walinzi getini, wahudumu wa mabasi na askari usalama wa barabarani.

Darasa lingine ni haja ya kuwaelimisha wasafiri kila mara kupitia vipaza sauti safarini, madereva na wahudumu wa vyombo vya usafiri wahakikishe wanatoa elimu ya kila mara.

### WAZIRI AFYA

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Gwajima, anasema elimu itaendelea kutolewa kwa wananchi wakishirikiana na wadau wengine na atahakikisha vifaa vya kujikinga vinaendelea kuwapo katika maeneo mbalimbali nchini.


Anasema, pia wamejikita kuendelea kutoa elimu za umuhimu wa chanjo, ili wananchi wachanje na kupunguza maambukizi.

Waziri anasistiza kuwa elimu itaendelea kutolewa kwa wengi na itawafikia wale walio wasikivu.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Wabongo propaganda zetu zitatuponza!






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

TANZANIA inajulikana duniani kwa utajiri wa maliasili ambao imekuwa ikijivunia, pia unaochangia uchumi wake na kuleta maendeleo.

Kikubwa katika utajiri huo ni wanyama na malikale, ambazo zinavutia watalii kutoka duniani na kuliingizia Taifa kipato.

Kwa kulitambua hilo, juhudi nyingi zimekuwa zikielekezwa katika sekta ya utalii, kuweka mazingira na miundombinu rafiki na vivutio kuendelea kuvutia kwa kuvilinda.

Hiyo imesababisha kuundwa kwa taasisi mahsusi, kwa ajili ya kuhifadhi maliasili na kupambana na ujangili. Ujangili unahujumu wanyama kwa kuwawinda, ili kuvuna nyara; pembe, ngozi na hata nyama na ndiyo sababu hata adhabu dhidi ya majangili ni kubwa.

Bila shaka, baada ya kufikiria ni upi mchango wake kivitendo katika hilo, hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alikuja na ubunifu, akaamua kutoka ofisini na kwenda kwenye vivutio kuandaa filamu ya kitalii. Akaanzia Zanzibar, akaenda Bagamoyo, Pwani na hatimaye mikoa ya Kaskazini, iliyo maarufu kwa utalii.

Akifuatana na wapiga picha wa kigeni na wa ndani, bila shaka Royal Tour hiyo, itazaa matunda na kuitangaza nchi kwa upana wake, lakini itavutia watalii. Uamuzi wa Rais Samia na utekelezaji wake, hakika utamfanya kuacha alama isiyofutika katika historia ya uongozi wake, hususan kwa utalii.

Lakini, kama itatokea bahati mbaya isilipe, basi kutakuwa na vikwazo vilivyochangia, ingawa mgeni akisikia rais anashiriki promosheni kama hii, atawiwa shauku ya kuona imefanyikaje.

Na katika udadisi huo, atakuja nchini kutalii na kuchangia kitu katika uchumi wa Taifa. Hilo linawezekana na ndiyo matarajio ya Watanzania wengi wanaoitakia mema nchi yao.

Hata hivyo, mpango huo kuna mambo hayajakaa sawa kisiasa na hivyo kutishia kuathiri uchumi, kama hatua hazitachukuliwa sawia.

Mathalan katika barabara zetu mikoani huko, wapo wanaoweka mabango yasiyo na busara. Kwa mshangao mkubwa utajiuliza, iweje watu wenye akili timamu kuandika kwenye mabango, yanayoongoza watumia barabara kufuata sheria!

Muktadha huo unaendana pia na tukio la hivi karibuni la shambulizi lililosababisha mauaji Dar es Salaam, la mkazi wa jiji hilo, Hamza Mohammed kuua naye kuuawa.

Akaua polisi na mlinzi wa kampuni binafsi naye akauawa na polisi. Punde si punde, Polisi ikatoa taarifa kuwa Hamza ni gaidi. Si jambojema kwa utalii wetu.

Lakini, kana kwamba hiyo haitoshi, Rais Samia kuzindua chanjo dhidi ya UVIKO-19, akachanjwa na kufuatiwa na Watanzania wengine tena kwa hiyari, lakini eti wakaibuka baadhi ya wachache wazito ndani ya chama chake, kupinga na baadhi kutuhumu chanjo hizo.

Watu wanapewa hoja chanjo ni hatari kwa binadamu, inasababisha matatizo kama ya akili na zaidi ya hapo. Tujiulize, dozi zaidi ya milioni mpaka sasa ina wateja wangapi? Kuna tatizo mahali, watu ama wameshawishika na propaganda au hofu tu?

Wapiga propaganda wanajikita kutaka watu wasijitokeze kuchanja katika hoja ya kuisababishia Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa yasiyojachanja kisawasawa.

Hiyo maana yake ni nini? Propaganda dhidi ya chanjo ni wazi inaichafua Tanzania machoni mwa wageni. Pia, niseme angalu kuna la busara, Msajili wa Vyama vya Siasa, Mutungi, kakutanisha Polisi na vyama hivyo. Nampongeza, kaliona!

Je, kama tukichafuana au kuchafuliwa kwa haya ya ya ugaidi na kutochanja, si ni azma ya kuipa walakini ufanisi wa utalii wetu. Tuumizwe vichwa na swali, nani atakuwa tayari kuja kuwekeza nchini mwetu? Je, nani atatambua juhudi za Rais Samia kuitangaza nchi kitalii? Alamsiki!

BIASHARA

# Zanzibar inavyoibuka upya kinara mzalishaji, muuzaji viungo duniani

• EU yaungana nao, kinamama kicheko • Soko liko kona zote, kazi kwao ubora



Wakulima wa kilimo mradi wa viungo kinachofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU), wakiwa na mbegu baada ya kukabidhiwa shambani kwao kijijini Kizimbani, Mkoa wa Magharibi Unguja. Mradi unalenga kuwawezesha kinamama wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JINA la Zanzibar la kisiwa cha marashi ya karafuu kinatokana na uzalishaji wa viungo mbalimbali vikiwamo karafuu, vanila na pilipili manga, ambavyo vimekuwa vivutio vya wageni wanaofika Zanzibar.

Katika miaka kati ya 1957 kabla ya uhuru hadi 1970, Zanzibar ilikuwa maarufu kwa usafirishaji na uzalishaji mazao hayo ya viungo katika bara la Afrika hadi Asia na kupewa jina "Spice Island".

Serikali iliyoko madarakani hivi sasa imekuja na mikakati katika sekta ya uzalishaji mazao ya viungo na kurudisha hadhi ya visiwa hivyo katika uzalishaji na usafirishaji mazao hayo duniani, yakiwa na bei yake katika soko la dunia.

Wataalamu wa biashara wanasema ni hatua inayowainua wakulima na kuwahakikishia maendeleo ya kiuchumi.

### ZIARA BALOZI EU

Hivi karibuni Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, aliutembelea mradi wa viungo, unaofadhiliwa na nchi yake ukitekelezwa visiwani Zanzibar namna wakulima na wakazi wengine walivyoonyesha utayari kutekeleza.

Balozi Fanti alizuru katika mradi huo Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kuzungumza na wakulima ambao wapo tayari katika utekelezaji, dhima kuu ni kuwakomboa vijana na wanawake ili wasonge mbele kiuchumi.

> **"Tumejipanga kurudisha hadhi ya Zanzibar kuwa kisiwa kinachoongoza kwa uzalishaji na usafirishaji mazao ya kilimo ya viungo, ambayo soko lake lipo kubwa na la uhakika nje ya nchi.**

Anasema kilimo cha viungo kina nafasi kubwa ya kubadilisha maisha ya wakulima kwa kuingia katika kilimo cha biashara na kusafirisha mazao hayo katika soko la dunia.

Balozi anawataka walengwa hao wa kilimo kupata mafunzo na ushauri wa mabwana na mabibi shamba, lengo ni kuongeza tija ya uzalishaji mazao ubora na kuingia katika soko la ushindani.

"Nimefurahishwa na kuona wakulima wengi walivyohamasika kulima kilimo cha mazao ya viungo, ambacho soko lake lipo kubwa la uhakika ndani na nje, hatua ambayo itabadilisha maisha ya wananchi kuwa bora," anasema.

### WAKULIMA

Mmoja wa wakulima wa mazao ya viungo vya vanilla, Haji Abdalla Abeid, anasema elimu aliyoipata kwa kiasi kikubwa imesaidia kuleta mabadiliko makubwa na matunda ameanza kuyaona.

"Nimefanya shughuli za kilimo hiki kwa miaka mingi, lakini kwa njia za kienyeji zaidi ambazo hazikuniwezesha kupata mafanikio mazuri, ikiwamo mavuno. Lakini sasa nimepata elimu ya kitaalamu na mabadiliko yake nimeanza kuyaona hatua kwa hatua,"anaeleza.

Anabainisha kuwa, amejifunza njia mpya za kilimo hicho cha vanila na tayari ameshaanza kuzifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha shamba jipya, aliloatesha miche zaidi ya 200.

Kuhusu soko, mkulima huyo anasema vanila huuzwa kwa bei kilo moja Sh. milioni 1.6 kupitia mradi wa kilimo cha mazao ya viungo na matarajio yake, soko hilo litaimarika zaidi.

Mkulima wa matunda, Asha Haji, aliyejikita katika Shehia ya Binguni Wilaya ya Kati Unguja, anaisema mfumo mpya wa kilimo unaozingatia elimu, utawaletea tija katika uzalishaji wao bidhaa mbalimbali.

Asha anayelima zaidi papai na pesheni, anasema kupitia mfumo huo mpya, anaamini watakuwa na uhakika wa soko kutokana na kuzalisha bidhaa bora zenye kiwango zitakazoingia katika ushindani wa soko la nje na ndani ya nchi.

"Matarajio yangu kilimo cha matunda kinaweza kuleta mabadiliko makubwa ya maisha yangu, kutokana na ubora wa bidhaa ninazozizalisha na kuingia katika ushindani wa soko," anasema.

Fatuma Hamadi, mkulima wa viungo na mboga, anazipongeza asasi za kiraia zilizoleta mradi huo kwa ukombozi wenye mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

"Mimi nimejipanga vizuri kujikita katika kilimo cha mazao ya viungo katika shamba langu. Nimekusudia kuanza kwa kulima vanila ambayo bei yake ni kubwa na soko lake lipo la uhakika," anatamka.

### WADHIBITI MRADI

Meneja wa Mradi wa Mazao ya Viungo, Amina Ussi Khamis, anasema wakulima wamejipanga kukipokea kilimo hicho chenye matarajio makubwa kubadilisha mfumo wa kilimo chao cha awali.

Kwa mujibu wa Meneja Amina, hivi sasa wanafuata maelekezo ya kitaalamu kwa ajili ya kupata mazao bora yatakayohimili mahitaji ya soko lenye ushindani mkubwa.

Akitoa taarifa za mradi huo, anasema wamelenga kuwafikia zaidi ya wakulima 57,974 asilimia 55 ni wanawake waliopo vijijini na mjini. Anasema mradi huo utawafikia moja kwa moja wakulima 21,000 wa mboga mboga, viungo na matunda.

Meneja anasema kuwa kuna asilimia ya wananchi watakaonufaika kupitia 'mnyonyoro wa thamani' ikiwamo wafanyabiashara watakaouza na kusafirisha mazao.

"Huu ni mradi mkombozi kwa wanawake kuanzia waliopo vijijini hadi mjini, ambao watalima mazao ya viungo pamoja na matunda na mboga mboga na kulitumia soko liliopo ikiwamo la utalii,"anasema.

Ofisa Kilimo cha Mboga kisiwani Pemba, Sada Juma Segeja, anasema wamejipanga vyema kuona kilimo cha viungo kinapata mafanikio makubwa, ikiwamo ya watalamu kilimo kuwafikia wakulima hadi waliko.

Rai yake anawahimiza wataalamu hao wa kilimo, kiwafikia na kuwapa wakulima elimu zenye tija na kuzaa mafanikio makubwa.

### KUTOKA SERIKALINI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Dk. Islam Seif, anasema wamejipanga kuhakikisha Zanzibar inarudia zama za kuwa visiwa vilivyoongoza katika kuzalisha na kusafirishaji mazao ya viungo.

Anasema Zanzibar imejipanga vyema kurudisha zao la viungo la vanila, pilipili manga na pilipili kichaa, kwa sababu bei zake ziko na ya uhakika, katika soko la dunia.

"Tumejipanga kurudisha hadhi ya Zanzibar kuwa kisiwa kinachoongoza kwa uzalishaji na usafirishaji mazao ya kilimo ya viungo, ambayo soko lake lipo kubwa na la uhakika nje ya nchi," anasema.

Mradi wa viungo hadi sasa unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na unatekelezwa katika Shehia 60 za Unguja na Pemba, ukilenga kuwanufaisha watu 57,974.

Pia ni mradi unaosimamiwa kwa pamoja na taasisi za Uhifadhi wa Misitu Pemba (PDF),Taasisi ya Kusaidia Maendeleo katika Jamii (CFP) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar.





# REA yaibuka mwitikio mdogo wa wananchi

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

KUTOKANA na kuwapo kwa mwitikio mdogo wa wananchi kuunganisha umeme vijijini, Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imekiagiza kitengo cha uhamasishaji kuweka jitihada katika kutoa hamasa kwa wananchi kuchangamkia fursa hiyo.

Mjumbe wa Bodi hiyo, Mhandisi Styden Rwebangila, aliyasema hayo wilayani hapa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili.

Alisema licha ya serikali kuwekeza fedha nyingi katika miundombinu ya umeme katika maeneo ya vijijini bado ipo shida kwa wananchi kutounganisha huduma hiyo katika nyumba zao.

"Sisi Bodi tumekuja kutembelea miradi hii ya REA lengo likiwa ni kuangalia maendeleo yake, lakini pia kuona kama huduma hii ambayo serikali imewekeza fedha nyingi kuweka miundombinu kama inawanufaisha wananchi," alisema.

Aidha, alisema kutokana na ziara hiyo, wamebaini bado wananchi wengi hawajanufaikiwa na huduma hiyo licha ya miundombinu ya umeme kupita jirani na makazi yao.

"Changamoto hii tumeiona na sisi kama Bodi tunakiangiza kitengo cha uhamasishaji kuja huku kwa wananchi ili kutoa hamasa kwa wananchi kuchangamkia fursa hii ya kuunganishiwa umeme kwani yapo baadhi ya maeneo ambayo wananchi wanalia kufikiwa na miundombinu hii," alisisitiza.

Pia, alisema katika miradi ya ujazilizi awamu ya pili A, zaidi ya vitongoji 349, vya Mkoa wa Dodoma vitanufaika kwa kufikishiwa huduma hiyo ya nishati ya umeme.

"Bodi pia tumeridhishwa na kasi ya mkandarasi kwani hadi sasa imefikia asilimia 64 ya mradi na kuvuka lengo ambalo lilikuwa ni asilimia 48, hadi kufikia sasa,"alisema.

Naye, Meneja Usimamizi Miradi ya REA, Mhandisi Romanus Lwena, aliwataka wananchi kuchangamkia fursa ya kuunganisha umeme ili kuanzisha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato.

"Umeme ni maendeleo serikali imewekeza kiasi kikubwa sana cha fedha katika kufikisha miundombinu katika maeneo mbalimbali hivyo wananchi hawanabudi kuchangamkia fursa hii na gharama ni kidogo kwa sasa ni Sh. 27, 000," alisisitiza.

Kaimu Meneja wa Tanesco Mkoa wa Dodoma, Donasian Shamba, alisema wamepokea maelekezo yaliyotolewa na Bodi na watayafanyia kazi kwa kuhakikisha wananchi wote waliofikiwa na miundombinu wanapata umeme.

Hata hivyo, Mkandarasi wa mradi, Mhandisi Sangora Mollel, alisema hivi sasa hawana changamoto kubwa zinazoweza kuwakwamisha kukamilisha mradi huo kwa wakati mwezi Aprili mwakani.




Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu maonyesho ya kwanza ya Utalii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kufanyika Oktoba 9 hadi 16, mwaka huu, jijini Arusha kwa kushirikisha nchi wanachama na wafanyabiashara wa ndani na nje. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yajivunia sera mpya ya vijana

**Na Peter Mkwavila** DODOMA

SERIKALI imesema sera mpya ya vijana itasaidia kuwawezesha kujiajiri na kukabiliana na tatizo la ajira nchini.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda, aliyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa vijana wa kuthibitisha Rasimu ya Sera hiyo ambao uliowashirikisha vijana 119 kutoka mikoa 22 nchini na maofisa maendeleo ya vijana 21.

Alisema maendeleo ya taifa yanachangiwa na sehemu kubwa ya vijana, hivyo kupitishwa kwa sera hiyo kutasaidia ustawi wao.

"Kupitia Sera ya mwaka 2007 tuliona kuna umuhimu wa kufanya mapitio kuendana na hali ya sasa... pia sera hii imepitiwa na wadau wa maendeleo na kujadiliana ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwani ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kunakuwa na mfumo rafiki na imepitiwa mikoa takribani 13 ikiwamo Pwani, Kigoma, Arusha, Dar es salaam, Mwanza na mingine,"alisema.

Katibu huyo alisema kuwa kutokana na mapitio ya sera hiyo Serikali inatarajia kuweka mikakati ya kimataifa ya dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 itakayojenga misingi imara ya kuwezesha vijana kutekeleza mambo yao na kushiriki katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

"Sera hii ijenge misingi ya umoja, mshikamano, uadilifu na uzalendo kwa vijana kupennda nchi yao tunafahamu wakijengwa hivi watakuwa tayari kupigania Taifa lao na hawatakuwa tayari kuona linachafuliwa," alieleza Nzunda.

Hata hivyo, alisema kuwa sera hiyo ielekeze ubunifu kwa vijana kubadilisha mtazamo wa nchi pamoja na kujenga ujumuishi ndani ya sera bila ubaguzi kwa maslahi ya taifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, James Kajugusi, alisema lengo la mkutano huo ni kupokea maoni ya vijana na maofisa vijana wa mikoa kwa niaba ya wenzao nchi nzima kuhakikisha kuwa sera hiyo inakuwa yenye tija na sehemu ya kutatua kero zinazowakabili.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo kutoka Mkoa wa Arusha, Debora Mlai, aliishukuru serikali kwa kuwashirikisha vijana katika uaandaji sera hiyo ili kutambua mchango wao.

## Mtaka ataka mikopo kwa wanawake

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameitaka Benki ya Biashara (TCB) kuwakopesha wanawake ili kujiepusha na 'mikopo umiza' ambayo imekuwa ikisababisha kuporwa vyombo vya ndani wanaposhindwa kurejesha.

Mtaka aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kongamano la wanawake wajasiriamali na wasio wajasiriamali la kukuza uchumi wa taifa lililoandaliwa na benki hiyo.

Alisema ni vyema mikopo ambayo wanakopeshwa wanawake hao imekuwa na riba kubwa na kusababisha kushindwa kufanya marejesho na kufilisiwa vitu vyao vya ndani.

"Mnapaswa mjitathmini vizuri kwanini wanawake wengi na jamii kwa ujumla wanakwenda kukopa mikopo umiza ambayo ina riba kubwa badala ya kukopa benki ambako kuna usalama katika mikopo wanaenda kuchukua," alisema.

Alisema uongozi huo unapaswa kuchunguza sababu za watu kukimbilia mikopo hiyo yenye riba kubwa na kuwa na wateja wengi hususan wanawake.

"Mkifanya uchunguzi wa kujua nini wale wa mikopo ya pembeni wanafanya mtafanikiwa kuchukua wateja wote na hapo sasa ndio mtaonyesha nini maana ya kuichukua benki ya wanawake kwa sababu mtakuwa mnawasaidia mikopo," alisema Mtaka.

Aidha, alisema TCB inapaswa kuangalia fursa za miradi inayotekelezwa na serikali, mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bomba la mafuta ili kuwakopesha fedha wanawake waende kupata nafasi za kuendesha biashara katika miradi hiyo.

"Rais Samia Suluhu alisema asilimia 30 ya miradi wanapaswa kupewa wanawake ili kujiinua kiuchumi, kuna umuhimu wa kufanya kazi kwenye miradi hii."

"Benki tafuteni fursa katika miradi ya serikali ili mpate nafasi ya kuwakopesha wanawake, niwaambieni tu wanawake ni wateja wazuri sana," alisema Mtaka.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa TCB, Sabasaba Moshingi, alisema malengo ya kongamano hilo ni pamoja na kutaka kuwasaidia wanawake kukua kiuchumi.

"Haya yaliyosemwa na Mkuu wa Mkoa sisi kama benki tutakaa na kuona nini tufanye ili kuwakusanya wanawake wengi na kutoa mikopo itakayowainua kiuchumi," alisema.

Kwa upande wake, mjasiriamali Rosemary Haule, aliishukuru TCB kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha mikopo inatoka kwa wakati na imesaidia kuendeleza biashara zao za kila siku.



# Wakurugenzi REA wawanyima makandarasi muda wa ziada

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

BODI ya wakurugenzi wa Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA), imepiga marufuku makandarasi waliopewa tenda ya kusambaza umeme kwenye vitongoji wanaoshindwa kukamilisha kazi zao kwa mujibu wa mikataba yao.

Badala yake imeagiza makandarasi hao wachukuliwe hatua kwa mujibu wa masharti ya mikataba hiyo.

Wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi wa REA juzi walifanya ziara katika Wilaya ya Kyela yenye lengo la kukagua utekelezaji wa mradi wa kusambaza vitongoji mkoani humo ambapo walipokea taarifa yenye kukatisha tamaa.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Romanus Lwena, alisema katika Mkoa wa Mbeya Kampuni inayotekeleza mradi huo wa usambazaji wa umeme vijijini inaitwa SAGECOM na kwamba waliingia nayo mkataba mwaka 2020.

Alisema mkandarasi huyo alianza kazi Machi 10, na kwamba kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi huyo anatakiwa kukamilisha kazi Desemba mwaka huu.

Hata hivyo, Mhandisi Lwena alisema mpaka sasa mkandarasi huyo amebakiwa na miezi mitatu pekee kwenye mkataba wake lakini utendaji kazi umefikia asilimia 25 pekee hali ambayo inatia wasiwasi endapo atamaliza.

"Kwa muda aliotumia ilitakiwa awe angalau amefikia asilimia 60 ili angalau kazi iwe inatia matumaini lakini mpaka sasa amefikia asilimia 25, mpaka sasa kuna baadhi ya vifaa bado hajaleta jambo ambalo linakatisha tamaa," alisema Mhandisi Lwena.

Alisema Mkandarasi huyo amepewa kazi ya kusambaza umeme kwenye vijiji zaidi ya 150 vya Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya lakini vijiji vingi bado mkandarasi huyo hajafika.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa REA walionyesha kukerwa na mwenendo wa mkandarasi huyo na hivyo wakatoa msimamo wa kutokumuongeza muda mkandarasi huyo pamoja na wengine waliopewa kazi hizo.

Mmoja wa wajumbe hao, Mhandisi Styden Rwebangira, alisema kufikia Disemba kama mkandarasi huyo atakuwa hajakamilisha kazi, hakuna kumuongeza muda, badala yake masharti ya mkataba wake yafuatwe kama yalivyo.

Alisema awali wakati wanawatumia wakandarasi wa ndani walikuwa hawawachukulii hatua za aina yoyote kutokana na wengi kuwa wachanga, hivyo walikuwa wanalelewa lakini kwa sasa wameshakuwa na wana ushindani mzuri.

"Baada ya mkataba wa mkandarasi huyu kuisha hakuna kumuongeza muda, tulikuwa tunawalealea, lakini kwa sasa kama ni mbeleko imeshafunguliwa na wanatakiwa watembee wenyewe kwa miguu yao na wana ushindani mzuri sana hivyo hakuna kuleana tena," alisema Rwembangira.

Alisema kwa sasa Serikali inahitaji Sh. trilioni 8.8 ili kumaliza kuunganisha umeme kwenye vitongoji vyote nchini, na kwamba mpaka sasa Serikali inapata Sh. bilioni 400 kwa mwaka mzima hali ambayo inatakiwa nguvu ya ziada.

Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Elisa Kirimbo, alisema Shirika hilo litahakikisha linamsimamia Mkandarasi huyo ili kuhakikisha anamaliza kazi hiyo kwa wakati.

Alisema mbali na mkandarasi huyo ambaye anafanya kazi ya kujaziliza umeme kwenye vijiji ambavyo vina umeme lakini kuna nyumba zilirukwa pia yupo mkandarasi ambaye anaunganisha kwenye vijiji ambavyo havina umeme kabisa.

Mwakilishi wa kampuni ya SAGECOM inayotekeleza mradi huo, Mhandisi Stanley Mwakabungu, alisema watahakikisha wanakamilisha kazi kwa muda uliopangwa.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiamaji wa Bonde Dogo la Mto Mbalizi, Aron Dauson (mwenye suti ya bluu), akizungumza kabla ya kukabidhi miche wa miti kwa wananchi wa Mji wa Mbalizi, mkoani Mbeya juzi, kwaajili ya kupandwa kwenye vyanzo vya maji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanafunzi waomba kupimiwa udongo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa Chuo cha Kilimo cha Mbalizi Polytechnic College, wamewaomba wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, kuwasaidia kupima afya ya udongo chuoni hapo ili kuendeleza uzalishaji wa miche ya mazao kwa ubora unaotakiwa.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Getrude Mbembati alisema hitaji lao kwa sasa ni kupimiwa afya ya udongo chuoni hapo kwa ajili ya kuzalisha miche ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda na baadae kuiuza kwa jamii inayowazunguka.

Alisema hadi sasa TARI -Uyole wamewapatia miche na mbegu za aina mbalimbali huku wakiwapatia elimu ya namna ya kuotesha na kuhudumia mimea hiyo.

"Tunawashukuru Kituo cha Uyole kwa kutupatia elimu kilimo bora pamoja na miche ambayo tunaendelea kuitunza hapa chuoni kwetu, jambo la muhimu kwa sasa ni kuomba wataalam kupima udongo wa hapa ili kufahamu ni aina gani ya mbegu au miche inayostahili kupandwa hapa lakini pia tukibaini tatizo mtatusaidia kutengeneza afya ya udongo," alisema Mbembati.

Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema walibaini tatizo kubwa kwenye afya ya udongo hivyo wameanzisha mradi wa kupima udongo katika mikoa minne ikiwamo Mbeya, Rukwa na Morogoro.

Alisema wataalam wa kituo hicho watakuwa wanapima udongo ili kujua tatizo lililopo pamoja na kutoa ushauri wa kitalaam kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mkuu wa Chuo cha Mbalizi Polytechnic College, Essau Mwasegile, alisema wamewajengea wanafunzi uwezo wa kuzalisha mbegu za aina mbalimbali na namna ya kuhudumia.

Alisema wamewajengea uwezo wa kwenda kuwafundisha wakulima namna bora ya kilimo bora pamoja na kuwapatia ushauri pindi wanapokabiliwa na matatizo katika uzalishaji.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, Gidion Malifimbo, alisema kwa sasa ana uwezo wa kutoa ushauri wa kilimo chenye tija kwa jamii yake na kwamba atakuwa mkulima wa mfano kwani atazalisha kwa kuzingatia utalaam.

# Wakazi jirani Mto Mbalizi waathiriwa majanga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wanaoishi pembezoni mwa Mto Mbalizi katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wako hatarini kukumbwa na majanga ya asili yakiwemo mafuriko, kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababisha uoto wa asili kutoweka.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya watumia maji wa Bonde Dogo la Mto Mbalizi, Aron Dauso, alisema bonde hilo limeharibiwa kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazofanywa kwenye mto huo ikiwamo uchimbaji wa mchanga.

Alizitaja shughuli zingine zilizochangia kuharibu bonde hilo ni kubonda kokoto kwa ajili ya shughuli za ujenzi, shughuli za ujenzi kwenye eneo la mita 60 kutoka kwenye mto pamoja na shughuli za kilimo kwenye maeneo hayo.

Alisema uharibifu huo wa mazingira unasababisha uwapo wa hatari kwa wanaoishi kwenye maeneo ya jirani na mto huo kukumbwa na mafuriko, ukame na matatizo ya uchafuzi wa maji ya kutumia majumbani.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, wameanza kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti kwenye kingo za mto huo kwa kushirikiana na wananchi wa vijiji husika.

"Mpaka sasa tumehifadhi mazingira kwa kushirikiana na wananchi kwenye vijiji 12 na tunaendelea kufanya shughuli hiyo kwenye vijiji vingine na tunapata ushirikiano mzuri kutoka kwa wananchi wa vijiji hivyo," alisema Dauson.

Alisema mpaka sasa wameotesha miti zaidi ya 5,000 ambayo ni rafiki kwa vyanzo vya maji ambayo inatakiwa kusambazwa kwenye vijiji vyote pamoja na kwenye makazi ya wananchi wanaoishi jirani na mto huo. Mmoja wa wajumbe wa Bodi hiyo, Raphael Mwakalenga, alisema miti wanayopanda kwenye bonde hilo ni rafiki kwa vyanzo vya maji kutokana na kutunza unyevu na kuweka kivuli kwenye maeneo hayo ili maji yasikauke.

Alisema miti hiyo wanaipanda katika maeneo ya vijiji hivyo ili kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji vilivyopo kwenye maeneo yao.

Hatua zinazochukuliwa na jumuiya ya watumia maji wa bonde hilo, baadhi ya wadau wa maji kutoka mkoani Katavi waliamua kwenda kujifunza mbinu zinazotumika ili na wao wakazitumie kutunza vyanzo mkoani kwao.

Mmoja wa wadau hao, Martin Mbaku, alisema baada ya kujifunza namna Jumuiya hiyo ya watumia Maji wa Bonde la Mbalizi na wao wanaenda kuhamasisha wananchi wanaozunguka mito kupanda miti hiyo.

Alisema jambo la kuhifadhi vyanzo vya maji siyo jukumu la jumuiya za watumiamaji pekee bali ni jukumu la kila mwananchi na akasisitiza kwamba watahakikisha wanatoa elimu kwenye maeneo yao.

## SMZ yaendelea mchakato kutafuta wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inaendelea na mchakato wa kutafuta wawekezaji mbalimbali kuwekeza katika nishati mbadala ya umeme kwa ajili ya mahitaji ya uwekezaji na viwanda.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Maji na Nishati, Suleiman Masoud Makame, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Welezo kwa tiketi ya CCM, Hassan Khamis Hafidh, aliyetaka kujua mchakato wa serikali kupata nishati mbadala kwa matumizi yake na kuacha kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara TANESCO.

Alisema suala la upatikanaji wa nishati mbadala limepewa kipaumbele cha kwanza katika serikali ili kuyafikia malengo ya uchumi wa bluu ambao umejikita katika uwekezaji wa miradi mbalimbali.

Alisema tayari wapo wawekezaji mbalimbali ambao wameonyesha nia ya kutaka kuwekeza nishati mbadala ya umeme wa jua pamoja na mawimbi ya baharini.

Aidha alisema wapo baadhi ya wawekezaji ambao tayari wameonyesha nia ya kuwekeza katika miradi ya umeme wa upepo.

"Nataka niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba wapo wawekezaji mbalimbali wameonyesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa umeme mbadala kwa lengo la kuhakikisha tunakuwa na umeme wa kutosha utakaochochea uwekezaji," alisema.

Alisema nishati mbadala ni muhimu na nchi haiwezi kutegemea umeme pekee kutoka TANESCO.

Kadhalika, alisema chanzo kimoja cha umeme kutoka TANESCO hakitoshelezi mahitaji ya umeme zaidi katika safari ya kuelekea katika uchumi wa bluu na uwekezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya viwanda.

# Wawakilishi watofautiana kuanzishwa ofisi ya Mufti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wanawake wametofautiana kuhusu muundo wa muswada wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti huku wakisema si dhambi kwa wanawake kuingizwa na kushika nafasi katika taasisi hizo kwa ajili ya kushughulikia changamoto zinazowakabili moja kwa moja ikiwamo ndoa na talaka.

Wakichangia muswada wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalumu kutoka Pemba, Zawadi Amour Nassor pamoja na Mwakilishi wa Viti Maalumu Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdalla, wamesikitishwa na muswada huo ambao haumtaji kabisa mwanamke katika kushika nafasi zozote katika uongozi wa ofisi hiyo.

"Sitetei hoja mwanamke kuwa Kadhi au Maulamaa...tatizo sheria yote hii haijamhusisha mwanamke eti kwa kisingizio cha dini...tuache kusingizia dini kumtenga mwanamke katika dhana ya maamuzi," alisema Zawadi Amour Nassor, Mwakilishi wa Viti Maalumu wanawake Kaskazini Pemba.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema amesikitishwa na katika kamati zote katika sheria hiyo ikiwamo ya maadili haikumtaja mwanamke huku yakiwapo mambo mengi yanayomhusu ikiwamo migogoro ya ndoa, talaka. Akizungumza masuala ya ndoa na talaka na ni busara kuwapo kamati ambazo zitawahusisha katika kupata usuluhishi wa tatizo hilo ambalo katika siku za hivi karibuni limechukua kasi kubwa.

"Hata hizo enzi za kiongozi wa dini ya Kiislamu alikuwa akiwaambia watu kupata elimu ya usuluhishi wa mambo muhimu kwa kuwaelekeza waende kumuona mkewe bibi Aisha," alisema. Mwakilishi wa Viti Maalumu wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdalla, alisema sheria yote kuanzia mwanzo hadi mwisho haujamuhusisha wala kumtaja mwanamke katika masuala ya kijinsia na mambo ya msingi yanayowahusu wanawake.

Alisema huu sio wakati tena wa kuwabeza wanawake katika kuyafikia maendeleo ya kweli na katika sheria ya kuanzisha Ofisi ya Mufti yapo mambo mengi yanayowahusu wanawake ambayo ni busara kuwaingiza katika nafasi za uongozi.

"Mheshimiwa Spika jamani tuache kuwabeza wanawake katika masuala ya kimsingi yanayowahusu ikiwamo huu mswada wa ofisi ya Mufti ambapo mambo mengi ikiwemo talaka na ndoa... tunawapuuza wanawake wakati leo Rais wa Jamhuri ya Muungano ni mwanamke," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulatif Yussuf, aliwataka Wawakilishi kuacha kuchanganya masuala ya dini na siasa. Alisema katika muundo wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti kwa asilimia mia moja unahusisha masuala ya Dini ya Kiislamu na yapo mambo hayawahusishi wanawake katika uongozi ikiwamo kusalisha pamoja na kufungisha ndoa.

"Mheshimiwa Spika muswada huu unahusisha moja kwa moja masuala ya dini ya Kiislamu ambapo tunapaswa kuwa makini sana na yapo mambo hayawahusishi wanawake...mimi sijasikia kuwapo kwa Mtume mwanamke au mwanamke kuozesha," alisema.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi Zanzibar, Riziki Pemba Juma, akipata chanjo ya ugonjwa wa corona kutoka kwa mtaalamu wa afya, katika Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar jana. Chanjo hiyo, inatolewa kwa ajili ya wawakilishi na wafanyakazi wa baraza hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# NMB kudhamini tamasha rasilimali vyakula baharini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imetangazwa kuwa mdhamini mkuu wa Tamasha la Rasilimali na Vyakula vya Baharini Visiwani Zanzibar (Zanzibar Sea Food Festival 2021), linaloratibiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Tamasha hilo la siku mbili linatarajiwa kufunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Oktoba 8, mwaka huu, katika fukwe za Kendwa, ambalo litawakutanisha wasanii wa kitaifa na kimataifa na wananchi zaidi ya 30,000, chini ya kaulimbiu, isemayo 'Kamata Mshipi, Vumba ni Fursa.'

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tamasha hilo, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard, alisema Beni hiyo inathamini jitihada za Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha uchumi wa bluu na kwamba dhamira ya dhati ya kuunga mkono jitihada hizo zimewachochea kukubali kudhamini tamasha hilo linaloenda kuongeza thamani ya utalii visiwani humo.

"Tunashukuru sana kwa fursa hii adhimu ya kuwa wadhamini wakuu wa tamasha hili la rasilimali na vyakula vya Baharini, hii ni kwa sababu NMB inathamini sana sekta ya utalii nchini na kwa kuthibitisha hilo, tumejikita zaidi kusaidia harakati za kufikia uchumi wa bluu, ambazo ziko chini ya Serikali ya Zanzibar," alisema meneja huyo.

Aidha, aliongeza kwa kusema "Kwa kuelewa umuhimu huo, wenyeji wetu ambao ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, ilipotuomba kudhamini, hatukusita kukubali tukitambua kuwa utalii unachangia uchumi, pamoja na asilimia 80 ya pesa za kigeni katika hazina ya serikali."

Alieleza kuwa wanaamini Zanzibar Sea Food Festival, lina umuhimu mkubwa katika kukuza utalii na kuchangia Pato la Taifa na wao kama wadau wa maendeleo, wanajisikia fahari kuwa sehemu ya mafanikio ya ukuzaji uchumi na kwamba wamejipanga vya kutosha kutumia kila fursa ya kusaidia mchakato huo.

Akilitambulisha tamasha hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema Zanzibar Sea Food Festival, limebuniwa kwa lengo la kusapoti juhudi za utekelezaji wa sera za Serikali ya Zanzibar, chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Aliyataja makundi yatakayoshiriki tamasha hilo kuwa ni pamoja na wavuvi, watalii, wasanii, wawekezaji, watembeza wageni, taasisi za fedha, mashirika ya teknolojia ya habari, mawasiliano, kampuni za vinywaji, hoteli za kitalii, migahawa na wananchi wa kada zote visiwani humo na Tanzania kwa ujumla.

"Faida mbalimbali zinatarajiwa kupitia tamasha hili, ambazo zitasaidia jamii ya wana Kaskazini Unguja, kama vile mauzo ya samaki na mazao ya bahari takribani tani 30, sanjari na kuwakutanisha na kuwaunganisha kibiashara wavuvi wasiopungua 10,000 na wawekezaji wa hoteli za kitalii wasiopungua 127," alisema. Alisema pia faida zingine zitokanazo na tamasha hilo ni ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa visivyopungua 150, ajira za muda 16,322, ujenzi wa barabara ya lami kilomita 2.5, maonyesho ya kazi za wavuvi na wajasiriamali, pamoja na kazi mbalimbali za uhifadhi wa mazingira.

Aliongeza kuwa tamasha hilo ambalo waratibu wenza ni pamoja na Clouds Media, Kampuni za STR8UP Vibes na Zan Ocean, litapambwa na burudani kutoka kwa wasanii wa kitaifa na kimataifa takribani 30, wakiwamo FireBoy wa Nigeria, Focalist na DJ Obza wa Afrika Kusini, na wakali mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU** KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 52/2019**

**(Asilia Shauri la Jinai Na. 294/2017, Mahakama ya Wilaya ya Mtwara)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA......................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**HAMISI MOHAMED KAZUMARI..............MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: HAMISI MOHAMED KAZUMARI – NAMYAMBA MTWARA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama kuu Mtwara kusikiliza rufaa hii mnamo tarehe 13/09/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.

Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi rufaa hii itasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28/7/2021.

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

116452102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 88/2019**

**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA**

**SHAURI LA MAOMBI NO. 11/2019**

**THE DPP..........................................APPELLANT**

**VERSUS**

**KASIMU ALLY................................RESPONDENT**

**KWA: KASIMU ALLY - MTWARA**

**KUITWA SHAURINI**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 13/9/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.

Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30/7/2021.

A.H. MSUMI
NAIBU MSAJILI MFAWIDHI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MTWARA

116452002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA NA.115/2020**

**(ASILIA JINAI 39/2020MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA.........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**MOHAMED SALUM KOWEKA.........MJIBU RUFAA**
**KUITWA SHAURINI**

**KWA,MOHAMED SALUM KOWEKA**
**C/O SHARIFA MOHAMED KOWEKA**
**SIMU 078774775/0787327958**
**BOX MIEMBENI**
**MTWARA**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 27/09/2021 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA ,BASI SHAURI HILI LITASIKLIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 02/09/2021

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

116451902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA 62/2019**

**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA JINAI NO.29/2017**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA .........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**AGNES SEVERINE.........MRUFANIWA**

**DADI SALUM NAMKUDU.......MRUFANIWA**

**KWA.AGNES SEVERINE**
**MBAE MASHARIKI**
**MTWARA**
**DADI SALUMU NAMKUDU**
**MAGOMENI 'B'**
**MTWARA**
**KUITWA SHAURINI**

HII NI KUWATAARIFU KUWA MNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUTAJWA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 20/09/2021 SAA2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA,BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 28/09/2021

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI MFAWIDHI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MTWARA

116451802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**Mwalimu Hassani Sinani**

Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari aina ya **SCUDO**, Inayotambulika kwa majina ya Adhifa M.Nabahani. Gari Yenye usajili **T 245 AHQ,** Chasis namba **TD 01W117585** na Engine namba **G 16A255604.** Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **LIN/RB/436883/2021.**

116451602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi No 87/2021**

**Ombi la ESTER HERON MNG'ANGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu CLEMENT ISDORY KIHEDE**

**KWA YEYOTE YULE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 04/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 08/09/2021.

Tarehe 08/09/2021

Sahihi ya Hakimu

116451502

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 35 YA MWAKA 2021**

**LETSHEGO BANK (T) LTD ...................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **2M INVESTMENT LIMITED ........................ WAJIBU MAOMBI**
2. **DONATHA LUCAS NYALLU**
3. **MARTIN DE SOUZER**

**KWA: 1. 2M INVESTMENT LIMITED**
**2. DONATHA LUCAS NYALLU**
**3. MARTIN DE SOUZER**

**KWA: POPOTE MLIPO**

Mahakama hii inawafahamisha kwamba mdai amefungua madai dhidi yenu nakala yake inapatikana katika mahakama hii.
Shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 04/10/2021 saa 2:30 Asubuhi mnatakiwa kuwepo au kuwakilishwa Kisheria Pamoja na Kuleta utetezi wenu dhidi ya madai haya.
Zingatia kwamba kutokufika kwenu tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya nyinyi kuwepo, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa leo hii mbele yangu na Mhuri wa Mahakama tarehe 02/09/2021

HAKIMU MKAZI
MWANZA

116450502

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**SHAURI LA MAOMBI NAMBA 45 YA MWAKA 2021**

**(Asilia Shauri la Madai na 23/2021)**

**LETSHEGO BANK (T) LTD ..................................... MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **RAIYA MOHAMED HAMAD .................................... WAJIBU MAOMBI**
2. **YUSUPH RAZAK LADHA**

**KWA: 1. RAIYA MOHAMED HAMAD**
**3. YUSUPH RAZAK LADHA**

**POPOTE MLIPO**

Mahakama hii inawafahamisha kwamba Mwombaji amefungua maombi dhidi yenu nakala yake inapatikana katika Mahakama hii.
Shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 15/09/2021 saa2:30 Asubuhi
Mnatakiwa kuwepo au kuwakilishwa Kisheria pamoja na kuleta utetezi wenu dhidi ya maombi haya.
Zingatia kwamba kutokufika kwenu tarehe hiyo, Shauri litaanza kusikilizwa bila ya nyinyi kuwepo, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa leo hii Mbele yangu na Mhuri wa Mahakama tarehe 01/09/2021

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI
MWANZA

116450602

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... OF 2021**

**In the matter of the estate of the late SPECIOZA PAUL MALEMBEKA Of Salimini within Dodoma City**

**And**

**In the matter of the application for letters of administration by DR MARCO MACHALO**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30 day of 09 2021.
**Dated at Dodoma this 08 day of 09 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

116450302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi No 88/2021**

**Ombi la ZAKARIA D. MTEVELE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu HAMISI JUMA NYEPELLELE**

**KWA YEYOTE YULE ANAYEHUSIKA POPOTE PALE**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/09/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 08/09/2021.

Tarehe 08/09/2021

Sahihi ya Hakimu

116450202

---

**K-FINANCE**

## MAJEMBE AUCTION MART

## TANGAZO LA NOTISI YA SIKU 14

KAMPUNI YA **K-FINANCE** IKISHIRIKIANA NA MAJEMBE AUCTION MART WANATOA NOTISI YA SIKU (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WAKOPAJI (WADAIWA) WAFUATAO

| NAMBA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI |
|---|---|---|
| 1. | JORDAN CHRISPIN KASSANGE | ALLY S. KHAMESSE |
| 2. | FRANCIS JEROME MAPUNDA | EUGINE MOYO |
| 3. | HANCE LAMECK MANJAWILA | HEROMINI |
| 4. | UTUKUFU ELIYA ADAMUWAPILI | CHRISTOPHER MPOKA |

WANATAKIWA KULIPA DENI LOTE NDANI YA MUDA ULIOTOLEWA IKIWA WATASHINDWA KULIPA NDANI YA MUDA TAJWA DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI WASILIANA NA NAMBA 0715980025, 0738165605 NA 0738165606.**

116451302

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.99 OF 2021**

**In the matter of the Estate of the late SELESTINA BENEDICT NHASA of Ipagala within Dodoma city**

**And**

**In the matter of the application for letters of administration by ALEX GEORGE MAKANGARA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **01 day of 10, 2021.**
**Dated at Dodoma this.... day of .......2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

116450002

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.95 OF 2021**

**In the matter of the Estate of the late MUSA JONAS MUNYALIVA of Ng'hong'honha Ward within City Council of Dodoma**
**and**
**In the matter of the application for letters of administration by SARAH ALOYCE MNYALIVA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **04 day of OCTOBER 2021.**
**Dated at Dodoma this 08 day of SEPTEMBER, 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY
PETITIONER
NGHONG'OHHA WARD
P.O BOX 1249
DODOMA

116450102

---

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Dunia inapokumbuka miaka 20 shambulio la kigaidi Septemba 11

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA matukio ambayo yaligubika uso wa dunia kwenye vyombo vya habari vyote miaka 20 iliyopita, ni shambulio la kigaini baada ya jengo pacha World Trade Center (WTC), lenye takribani ghorofa 220, jijini New York, Marekani kushambuliwa na kupoteza uhai wa watu wapatao 3,000.

Kesho ikiwa inatimia miongo miwili tangu shambulio hilo kutokea, wakati ndege mbili za Boeing 767 ya 'American Airlines Flight 11' na 'United Airlines Flight 175' kugonga majengo pacha (Twin Towers), tukio ambalo liliongeza hali ya kuimarishwa usalama duniani ikiwamo kukua kwa teknolojia za ulinzi za kisasa.

Baada ya shambulio hilo Septemba 11, mwaka 2001, Osama bin Laden, kiongozi wa kundi la Al-Qaeda alikuwa mmoja wa wanaosakwa zaidi huku Marekani ikitangaza dau kwa ambaye atasaidia kupatikana kwake.

Marekani iliamini kwamba, Osama ndiye mshukiwa mkuu wa mashambulizi hayo katika majengo yaliyokuwa marefu na pacha ya biashara eneo lililoitwa 'World Trade Center' jijini New York na makao makuu ya jeshi, Pentagon.

Wiki tatu baada ya shambulio hilo, Rais wa Marekani wakati huo, George W. Bush alitangaza rasmi kwamba, Oktoba 7, mwaka huo itaanza vita dhidi ya ugaidi na kuwasaka waliohusika na shambulizi hilo lililoua watu zaidi ya 3,000.

Osama bin Laden alikuwa nchini Afghanistan na kundi lake la Al-Qaeda, wakiungwa mkono na kundi la Taliban waliokuwa wanaongoza sehemu kubwa ya Afghanistan.

Baada ya miaka 10, Osama aliuawa Mei 2, mwaka 2011, mjini Abbottabad, nchini Pakistan katika operesheni maalumu iliyoendeshwa na vikosi vya Marekani, chini ya utawala wa Rais Barack Obama.

Osama, alihusishwa kwa karibu na shambulio hilo, ingawa Mohammed almaarufu KSM alivyokuwa akifahamika, ndiye alibainika ndiye mratibu mkuu, kwa mujibu wa Tume ya Uchunguzi ya 9/11 iliyochunguza mashambulizi hayo.

Ndiye mtu aliyekuja na wazo hilo na kulipeleka kwa Al-Qaeda.

Marekani, inafahamika ni taifa kubwa duniani kiuchumi na kwenye kila sekta kwa kuwa uwezo wake kifedha kunaifanya kuzatiti kila eneo, ikiwamo kwenye suala la majeshi ya ulinzi.

Pamoja na umaarufu huo tukio hili liliishangaza dunia na hata nchi yenyewe. Shambulio la Septemba 11, mwaka 2001 ni tukio kubwa kuwahi kuitingisha Marekani, likielezwa washambuliaji wa kujitoa mhanga kuteka ndege nne za shirika la ndege la Marekani na kuzitumia kushambulia kwa kuzibamiza kwenye majengo pacha na jengo la Pentagon, makao makuu ya jeshi.



Majengo pacha iliyokuwa World Trade Center (WTC) katika mwonekano wake kabla na baada ya kushambuliwa Septemba 11, mwaka 2001. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Majeruhi 10,000 walitokana na shambulio hili, mbali na kufanya operesheni ya kumsaka Osama pia zilifanywa nyingine nchi za Iraq na kuuondoa utawala wa Saddam Hussein.

### UMAARUFU WA JENGO PACHA WTC

Baada ya shambulio hilo, Septemba 11, mwaka 2001, majengo yote mawili ambayo yalikuwa marefu zaidi jijini New York, yalitoweka ndani ya sekunde, ingawa moto kwenye kifusi ulidumu na kuwaka kwa siku 100 takribani miezi mitatu.

Kadhalika muda wa kusafisha eneo hilo ulichukuwa miezi nane ikiwamo kuondoa vifusi vya majengo mengine ya pembeni ambayo pia yaliathiriwa na shambulio hilo.

Upande wa kaskazini wa jengo hilo lilishambuliwa majira wa saa 2:46:40 asubuhi, na shambulizi likitua ghorofa ya 93. Dakika 17 baadaye saa 3:03:11 asubuhi, ndege aina ya United Airlines Flight 175 ilitua kusini mwa jengo na kutua kwenye ghorofa ya 77 na 85.

Jumba hilo liliungua moto kwa takribani dakika 56 na ilipofikia muda wa saa tatu na dakika 59, lilianguka kwa sekunde tisa pekee.



### SABABU JENGO KUANGUKA

Profesa Eduardo Kausel, mhandisi wa umma katika Idara ya Uhandisi wa Kiraia na Mazingira katika Taasisi ya Teknolojia, anasema:

"Jibu lililokubaliwa na watu wote ni kwamba majengo pacha yalianguka kwa sababu lilikuwa shambulio la kigaidi."

Baada tu ya mashambulio hayo, Kausel alikuwa kiongozi wa utafiti na machapisho kadhaa, wataalamu kutoka BBC MIT walichambua sababu za maporomoko ya ardhi kutoka kwa muundo wa uhandisi na usanifu.

Utafiti wa MIT, ambao ulichapishwa mwaka 2002 na matokeo ya ripoti ya serikali ya Marekani baada ya kuagiza Taasisi ya Kitaifa ya Viwango na Teknolojia (NIST), kujua kwa nini majengo hayo yalianguka na toleo lake la mwisho lilichapishwa mnamo mwaka 2008.

Wote MIT na NIST wanahitimisha kuwa majengo pacha yalianguka haswa kwa sababu mbili zilizokwenda pamoja kwamba uharibifu mkubwa wa majengo uliosababishwa na ajali za ndege katika kila jengo na kiasi cha moto ambao ulienea kwenye ghorofa kadhaa.

"Kama kungekuwa hakuna moto, majengo yasingeanguka. Na ikiwa kungekuwa na moto tu, bila uharibifu wa majengo, yasingeanguka pia," anasema Kausel.

"Majengo yalikuwa na msingi imara," anasema mhandisi huyo.

Ripoti ya NIST, kwa upande wake, inasema kwamba kuna hati rasmi ambazo zinaonyesha kwamba majengo hayo yaliundwa kuhimili athari za ndege ya Boeing 707, ambayo ilikuwa ndege kubwa zaidi ya kibiashara iliyokuwapo wakati wa usanifu.

Watafiti wa NIST, hata hivyo, wanaonya kwamba hawakupata habari juu ya vigezo na njia ambazo zilitumika kufikia matokeo hayo. Kilicho wazi ni kwamba, pamoja, athari na moto ulitoa matokeo mabaya kuanguka kwa majengo yote mawili.

Majengo pacha yalikuwa na muundo ambao ulikuwa wa kawaida katika miaka ya 1960, yalipoanza kujengwa.

Kila jengo lilikuwa na vyuma vilivyo wima na saruji katikati, ambayo ilikuwa na lifti na ngazi.

Kila ghorofa iliundwa na safu ya mihimili ya chuma kwa usawa, ambayo ilianza kushikamana na nguzo za chuma kuunda kuta za nje za jengo hilo.

Mihimili ilisambaza uzani wa kila sakafu kuelekea nguzo, wakati kila sakafu, ilifanya kazi kama msaada wa pande zote ambao ulizuia nguzo kutikisika, ambazo katika uhandisi wa umma inajulikana kama 'buckling'.

Muundo wote wa chuma ulifunikwa na saruji, ambayo ilifanya kazi kama mlinzi wa mihimili na nguzo ikiwa kuna moto.

Mihimili na nguzo pia zilifunikwa na safu nyembamba ya kuzuia moto.

"Mtetemeko kutokana na mshtuko huo ulisababisha chuma kupasuka, na kuacha mihimili ikifunuliwa zaidi na moto," anaelezea Kausel.

Kwa hiyo, uharibifu wa kimuundo ulifanya moto kusafiri, ambao nao ulisababisha uharibifu zaidi wa muundo.

**KWA MSAADA WA MTANDAO**

MECHI KALI

HOME / AWAY

BRONDBY

1.82 | 3.70 | 3.90

SILKEBORG

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 482

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GRIEZMANN: MIMI NDIYE NIMETAKA KURUDI ATLETICO



**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya Antoine Griezmann kuifungia timu ya Taifa ya Ufaransa dhidi ya Finland katika mchezo wa kutafuta tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwaka 2022, na kumaliza ukame kwa timu ya Didier Deschamps kutoshinda mechi mbili, amefunguka kuhusu kurudi kwake Atletico Madrid.

Griezmann alifunguka akiwa kama mchezaji wa Atletico Madrid kwa awamu ya pili, na aliweka wazi kwamba anatarajia kuweka uhusiano mzuri na mashabiki wa klabu hiyo.

Ikiwa hiyo itafanyika mara moja haijulikani, haswa baada ya machafuko ambayo yalitokana na jinsi Griezmann alivyoondoka kwenda Barcelona.

"Nadhani kumekuwa na uhusiano mzuri sana kati ya mashabiki na mimi, nataka kuipata tena," alisema Griezmann akiwaambia waandishi wa habari.

"Nitatoa kila kitu kama ilivyokuwa kawaida ya uchezaji wangu uwanjani, nitatoa kila kitu kwa mashabiki ambao wako kwenye viunga na wanaangalia kwenye runinga.

"Tunatumaini kuwa tunaweza kusonga pamoja tena, hiyo ndiyo nia yangu kuu ya kufunga, niko hapa kutoa kila kitu."

Kocha Diego Simeone anajulikana kuwa na uhusiano mzuri na Griezmann, na mshambuliaji huyo alikuwa mwepesi kutoa shukrani zake kwa raia huyo wa Argentina.

# *Wachezaji nane wafungiwa EPL*

**LONDON,** England

BAADA ya kuwapo kwa hali ya sintofahamu muda mfupi baada ya klabu kadhaa za Ligi Kuu England, EPL, kutowaachia wachezaji kwenda kuzichezea timu zao za taifa, madhara yake yameonekana.

Takriban wachezaji nane wanaocheza Ligi Kuu England, watakosekana viwanjani kwa siku tano. Hii ni baada ya Shirikisho la Soka la Brazil, kulitaka Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kutekeleza sheria ya kuwafungia wachezaji ambao hawakuitikia wito wa kuitumikia timu yao ya taifa.

Ederson, Alisson, Gabriel Jesus, Fred, Fabinho, Firmino, Thiago Silva na Rafinha ni wachezaji ambao walipaswa kuitumikia Brazil, lakini kutokana na klabu zao kutowaruhusu kwenda Brazil, sasa watakaa nje ya uwanja kwa siku tano.

Inaripotiwa kuwa tayari Fifa imeshazitaarifu klabu za Manchester United, Manchester City, Liverpool, Chelsea na Leeds United, kuhusu hali ya wachezaji hao na hivyo klabu zinapaswa kufikiria mipango mingine ya kuendelea bila wachezaji hawa kwa siku tano.

Hili huenda likawa ni pigo kubwa kwa Man United ambao wanamkosa Scot McTominay (majeruhi) na sasa Fred katika safu yao ya kiungo.

## HABARI MICHEZO

,274,020 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/09/21 | 17:00 | Brentford vs Brighton | 2.72 | 3.12 | 2.72 |
| 02. 11/09/21 | 17:00 | Watford vs Wolverhampton | 3.27 | 3.17 | 2.30 |
| 03. 11/09/21 | 17:00 | Southampton vs West Ham | 2.87 | 3.42 | 2.42 |
| 04. 11/09/21 | 17:15 | Ternana vs Pisa | 2.46 | 3.07 | 2.92 |
| 05. 11/09/21 | 19:00 | Napoli vs Juventus | 2.56 | 3.46 | 2.66 |
| 06. 11/09/21 | 22:00 | Amorebieta vs Burgos | 2.42 | 2.95 | 3.10 |
| 07. 12/09/21 | 14:00 | Montpellier vs St Etienne | 2.44 | 3.38 | 2.79 |
| 08. 12/09/21 | 16:00 | Bordeaux vs Lens | 3.09 | 3.39 | 2.24 |
| 09. 12/09/21 | 16:00 | Brest vs Angers | 2.65 | 3.30 | 2.60 |
| 10. 12/09/21 | 16:00 | Spezia vs Udinese | 2.92 | 3.38 | 2.40 |
| 11. 12/09/21 | 17:15 | Osasuna vs Valencia | 2.51 | 3.07 | 3.02 |
| 12. 12/09/21 | 18:30 | VfL Bochum vs Hertha BSC | 2.93 | 3.23 | 2.41 |
| 13. 12/09/21 | 19:15 | Ponferradina vs Almeria | 2.80 | 3.30 | 2.41 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**IJUMAA - 10 - SEPTEMBA 2021**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1143 | Nagoya Grampus vs Tokushima Vortis | 1.74 | 3.17 | 4.87 |
| 13:30 | 2295 | Brisbane Knights vs MT Gravatt Hawks | 3.00 | 4.06 | 1.94 |
| 17:00 | 5779 | Sheffield United U23 vs Bristol City U23 | 2.11 | 3.65 | 3.20 |
| 17:55 | 5756 | FK Napredak vs Radnik Surduluca | 1.74 | 3.43 | 4.35 |
| 18:00 | 1752 | CS Mioveni vs Chindia Targoviste | 2.68 | 2.78 | 2.88 |
| 18:00 | 2345 | Zlate Moravce vs Ruzomberok | 2.46 | 3.47 | 2.50 |
| 18:00 | 3212 | Pribram vs Zbrojovka Brno | 2.76 | 3.20 | 2.38 |
| 18:00 | 4161 | Klubi 04 vs RoPs Rovaniemi | 2.86 | 3.29 | 2.27 |
| 18:00 | 4452 | SK Lisen vs Dukla Prague | 2.39 | 3.14 | 2.80 |
| 18:00 | 5376 | Tallinna JK Legion vs Tammeka Tartu | 1.49 | 4.27 | 5.24 |
| 18:30 | 1639 | TPS Turku vs Musa Pori | 1.24 | 5.42 | 9.68 |
| 18:30 | 4292 | IF Gnistan vs EIF Ekenas | 2.75 | 3.57 | 2.21 |
| 19:00 | 1690 | Jihlava vs Opava | 2.17 | 3.28 | 3.04 |
| 19:00 | 3120 | Midtjylland vs Nordsjalland | 1.52 | 4.33 | 5.31 |
| 19:30 | 1725 | Oleksandria vs FC Ingulets | 1.88 | 3.58 | 3.53 |
| 19:30 | 2137 | SV Horn vs FC Juniors OO | 2.05 | 3.63 | 3.00 |
| 19:30 | 5155 | Kapfenberg vs SV Lafnitz | 4.06 | 3.77 | 1.71 |
| 20:00 | 1277 | Spartak Subotica vs Backa Topola | 2.54 | 3.27 | 2.54 |
| 20:30 | 4341 | Lokomotive Sofia vs Pirin Blagoevgrad | 2.03 | 3.34 | 3.29 |
| 21:00 | 1569 | Roda Kerkrade vs NAC Breda | 2.00 | 3.65 | 3.22 |
| 21:00 | 2548 | SBV Excelsior vs Dordrecht | 1.35 | 5.08 | 6.84 |
| 21:00 | 2631 | Emmen vs Maastricht | 1.42 | 4.71 | 5.89 |
| 21:00 | 2716 | Jong PSV vs Jong Ajax | 2.26 | 3.67 | 2.69 |
| 21:00 | 2890 | Telstar vs Almere City | 3.17 | 3.66 | 2.01 |
| 21:00 | 2928 | FC Oss vs ADO Den Haag | 2.38 | 3.33 | 2.74 |
| 21:00 | 2968 | VVV Venlo vs Den Bosch | 2.15 | 3.57 | 2.94 |
| 21:00 | 3196 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Utrecht | 2.11 | 3.70 | 3.15 |
| 21:00 | 3252 | UTA Arad vs Rapid Bucuresti | 2.11 | 2.95 | 3.74 |
| 21:00 | 3715 | Brondby vs Silkeborg | 1.82 | 3.70 | 3.90 |
| 21:00 | 3988 | De Graafschap vs FC Volendam | 1.74 | 3.83 | 4.03 |
| 21:00 | 5062 | HNK Gorica vs Hrvatski Dragovoljac | 1.33 | 4.85 | 7.37 |
| 21:30 | 1092 | Benevento vs Lecce | 2.25 | 3.15 | 3.20 |
| 21:30 | 1175 | Bray Wanderers vs Athlone Town | 1.42 | 4.55 | 5.81 |
| 21:30 | 2063 | Yverdon-Sport FC vs FC Aarau | 3.49 | 3.88 | 1.81 |
| 21:45 | 1103 | Harrogate vs Newport | 2.05 | 3.38 | 3.38 |
| 21:45 | 1106 | Derry City vs Finn Harps | 1.94 | 3.24 | 3.68 |
| 21:45 | 1398 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 3.45 | 3.25 | 2.01 |
| 21:45 | 2502 | UCD Dublin vs Cabinteely | 1.42 | 4.55 | 5.81 |
| 21:45 | 2670 | Cork City vs Shelbourne | 3.82 | 3.29 | 1.89 |
| 21:45 | 2777 | Glentoran Belfast vs Ballymena Utd | 1.43 | 4.70 | 6.60 |
| 21:45 | 2834 | Galway United vs Treaty United | 1.55 | 3.84 | 5.24 |
| 21:45 | 4430 | Brugge vs Oostende | 1.35 | 5.11 | 7.28 |
| 21:45 | 5100 | Barrow vs Colchester | 1.97 | 3.24 | 3.78 |
| 21:45 | 5683 | Sligo Rovers vs St Patricks | 2.85 | 2.95 | 2.47 |
| 22:00 | 1659 | Wexford Youths vs Cobh Ramblers | 3.09 | 3.38 | 2.10 |
| 22:00 | 1663 | Shamrock Rovers vs Waterford Utd | 1.30 | 4.75 | 8.72 |
| 22:00 | 2947 | Sporting Gijon vs Leganes | 2.36 | 2.91 | 3.25 |
| 22:00 | 3129 | Birmingham vs Derby | 1.86 | 3.20 | 4.43 |
| 22:00 | 5065 | Lorient vs Lille | 3.58 | 3.33 | 2.06 |
| 22:15 | 1734 | CF Estrela vs Rio Ave | 4.30 | 3.42 | 1.79 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# AGUERO KARIBUNI KUICHEZEA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

MAJERAHA aliyoyapata Sergio Aguero yanaifanya Barcelona kuikosa huduma yake, lakini ameanza mazoezi madogo madogo tangu aanze kupata nafuu.

Aguero ambaye alijiunga na Barcelona akitokea Manchester City kwenye usajili huru wa majira haya ya joto, hadi sasa bado hajacheza mechi hata moja tangu ajiunge na miamba hao wenye makazi yao jijini Barcelona.

Barcelona inatarajia kupata huduma ya Aguero kuanzia katikati ya Oktoba ingawa inamuhitaji sana wakati huu kwani imepoteza wachezaji wake hatari kama Lionel Messi ambaye amesajiliwa na klabu ya Paris Saint Germain, huku Antonio Griezman akienda Atletico Madrid kwa mkopo.

Aguero amesaini dili la miaka miwili na miamba hiyo ya jijini Barcelona huku kukiwa na matarajio makubwa kwake kwa klabu hiyo, kwani alionyesha makali yake akiwa na Manchester City ambapo aliifungia mabao 184 katika michezo 277.

Aguero mwenye umri wa miaka 33, anatarajiwa kuendeleza makali yake akiwa na Barcelona japo anapitia kipindi cha majera ya mara kwa mara.



# Rudiger bado hakijaeleweka

**LONDON,** England

CHELSEA hawajafanikiwa kukamilisha mazungumzo ya mkataba mpya na mlinzi wao, Antonio Rudiger.

Klabu ya Chelsea inaripotiwa kuwa inakutana na kikwazo katika jitihada za kumshawishi Rudiger kusaini mkataba mpya.

Mlinzi huyo wa kati raia wa Ujerumani ambaye alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu chini ya kocha Thomas Tuchel- tayari ameingia kwenye miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake.

Kwa mujibu wa Daily Mail, ofa ya hivi karibuni ya Chelsea ya mkataba mpya wa Rudiger ilienda tofauti, huku maboresho zaidi yakishauriwa kufanyika kwenye mkataba huo.

Taarifa zinaeleza kuwa hali ya mkataba wa nyota huyo, mwenye miaka 28, inafuatiliwa na klabu kadhaa kubwa wakiwamo Real Madrid, Bayern Munich, Paris Saint-Germain, Juventus na Atletico Madrid.

Pia Tottenham Hotspurs wanatajwa kuwa wapinzani pekee wa Ligi Kuu England wanaojaribu kuonyesha nia ya kumtaka nyota huyo. Awali, Spurs walishajaribu kuinasa saini yake, lakini wakashindwa kufanikisha jambo hilo.

Wakati sekeseke la mkataba mpya wa Rudiger zikiendelea, hadi sasa nyota huyo amecheza zaidi ya mechi 150 na Chelsea tangu alipowasili klabuni hapo mwaka 2017.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# REAL MADRID SASA WAAMUA KUMGEUKIA LEWANDOWSKI

Ni kama watashindwa kumsajili straika wa kimataifa wa Norway, Haaland kutoka Dortmund...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inapanga kumsajili Robert Lewandowski kutoka Bayern Munich kama watashindwa kumchukua Erling Haaland kutoka Borussia Dortmund, kwa mujibu wa AS.

Straika huyo wa Dortmund, Haaland ni mmoja wa wachezaji wanaowaniwa sana na Madrid, lakini kama watashindwa kumsajili raia huyo wa Norway, watahamia kwa nyota wa kimataifa wa Poland, Lewandowski.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, tayari amefunga mabao matano katika mechi tatu za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu.

**Kwa kipindi cha msimu wa 2020-21, straika huyo alifunga mabao 41 kwenye ligi na kutoa mchango katika mabao saba.**

Msimu wa 2019-20, mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund alifunga mabao 34 na kutoa 'asisti' nne kwenye ligi.

Haaland mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao 27 na kutoa asisti sita kwenye Bundesliga, na kufunga mabao 10 na kutoa asisti mbili kwenye mechi nane za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Haaland pia amekuwa akihusishwa pia na Manchester City, Manchester United, Paris Saint-Germain, Juventus, Liverpool, Barcelona na Bayern Munich.

Madrid pia kwa muda mrefu wamekuwa wakihusishwa na nyota wa PSG, Kylian Mbappe.

Mbappe amekataa kuongeza mkataba mpya na PSG na hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu ujao.

## ZISIKUPITE

### RUDIGER ATAKIWA PSG

KLABU ya PSG inamtaka mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, ambaye mkataba wake na Chelsea umebakiza mwaka mmoja kumalizika. ***(Le10Sport)***

### UNITED WAMTAKA RICE

MANCHESTER United wamemtambua mchezaji wa kimataifa wa England na West Ham, Declan Rice, 22, kama chaguo lao la kwanza katika dirisha la uhamisho litakapofunguliwa majira ya joto yajayo. ***(Manchester Evening News)***

### CARVALHO AWANIWA MADRID

REAL Madrid na klabu kadhaa za Ligi Kuu England, zinamfuatilia kwa karibu mchezaji wa Fulham, Fabio Carvalho, 19. Mshambuliaji huyo wa Ureno, amebakiwa na mwaka mmoja katika mkataba wake kabla ya kuondoka hapo Uwanja wa Craven Cottage. ***(Mail)***

### BELLINGHAM, MKATABA MPYA

KLABU ya Borussia Dortmund imekubaliana juu ya mkataba mpya na kiungo wa England, Jude Bellingham, 18, na hawana mpango wa kumuuza mchezaji huyo msimu ujao licha ya kwamba ananyatiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England. ***(90Min)***

### KESSIE KUONDOKA MILAN

NYOTA Franck Kessie, 24, huenda akaondoka AC Milan Januari mwakani baada ya kiungo huyo wa Ivory Coast kukataa ofa ya mkataba wa euro milioni 6.5 kwa mwaka kutoka kwa klabu hiyo. ***(Tuttosport)***

### MESSI NA ARGENTINA

LIONEL Messi, 34, amesisitiza kuwa mkataba wake na Klabu ya Paris St-Germain unajumuisha kifungu ambacho kitamwezesha kumpa kipaumbele Argentina kwenye mechi za kimataifa. ***(Sport)***

### COUTINHO KUIJAZA NOTI LIVER

BARCELONA italazimika kuilipa Liverpool kiasi cha euro milioni 20 kama marupurupu ya ziada ikiwa Philippe Coutinho, 29, ataiwakilisha zaidi ya mara 100 klabu hiyo. Mchezaji huyo amecheza mechi 90.

### MENDY AGONGA MWAMBA

UHAMISHO wa mkopo wa kiungo wa kati wa Leicester, Nampalys Mendy, 29, kwenda Galatasaray umegonga mwamba kwa sababu mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal hawezi kufika Istanbul kabla ya dirisha la uhamisho la Uturuki kufungwa. ***(Foot Mercato via Get French Football News)***

### LUIZ AREJEA BRAZIL

MLINZI wa zamani wa Arsenal, David Luiz, 34, anapania kurejea nyumbani kwao Brazil baada ya kupuuza ombi la Marseille. ***(Le10Sport)***

### OZIL AWANIWA MLS, QATAR

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Mesut Ozil, 32, ananyatiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu Marekani (MLS) na Qatar baada ya mkataba wa kiungo huyo wa Ujerumani utakapomalizika Fenerbahce. ***(AS - in Spanish)***

## HABARI MICHEZO

## Biashara Utd yaingiwa hofu dimbani CAF leo

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KWA mara ya kwanza kwenye historia ya klabu ya Biashara United, leo inatarajia kucheza mechi ya kwanza ya michuano ya kimataifa tangu kuanzishwa kwake mwaka 1990, itakapokuwa ugenini dhidi ya Dikhil ya Djibouti.

Mechi hiyo inatarajiwa kuchezwa majira ya saa 11:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Biashara United, ambayo ilitarajiwa kuondoka jana saa 9:00 jioni, baada ya kushindikana juzi kwa baadhi ya wachezaji wake kukosa Visa, itacheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa, ikiwa ni ya Kombe la Shirikisho hatua za awali.

Kocha Mkuu wa timu hiyo yenye maskani yake mkoani Mara, Patrick Okumu, licha ya kuingiwa na hofu ya kufanya vizuri katika mchezo huo kutokana na changamoto zilizojitokeza za kuchelewa kuwasili nchini humo, amesema Biashara itacheza mechi hiyo kwa ajili ya Watanzania na siyo kwa watu wa mkoa wa Mara pekee.

Akizungumza na gazeti hili jana, kabla ya kuanza safari, alisema kuchelewa kwenda nchini humo kutawaghariмu kwani watafika siku ya mchezo na ukizingatia wachezaji watakuwa na uchovu kutokana na kuchoshwa na safari.

"Lazima itatuadhiri kwa sababu tunaondoka tukiwa tayari tumechelewa na tunatakiwa kucheza kesho (leo jioni) kwa upande wetu mchezo hautakuwa salama sana kutokana na sababu hiyo, tunaomba Mungu atufanyie wepesi,"alisema Okumu kabla ya kuondoka hapo jana.

# AZAM KUWAVAA WASOMALI LEO BILA MASHABIKI, DUBE

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF), Azam FC, wakishuka dimbani leo kucheza dhidi ya Horseed ya Somalia bila uwapo wa mashabiki uwanjani, pia watakosa huduma ya straika wake hatari, Prince Dube, ambaye ni majeruhi, imeelezwa.

**Uongozi wa klabu hiyo, Azam FC umeweka wazi kwamba umepokea taarifa kupitia Shirikisho la Soka nchini (TFF) kutoka Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) juu ya kutokuwapo kwa mashabiki uwanjani kwenye mechi yao dhidi ya Horseed FC ya Somalia.**

Azam FC itawakaribisha Wasomalia hao katika mchezo huo wa awali wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaopigwa katika Uwanja wao wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabiti 'Zaka Zakazi', alisema hawana jinsi kutokana na taarifa hizo kutoka CAF, kwa sababu hali hiyo ni kutokana na changamoto za ugonjwa wa COVID-19 ambao dunia nzima inakabiliana nao kwa sasa.

Alisema kikubwa waliendelea kufanya maandalizi mazuri baada ya wachezaji wote walikuwapo kwenye majukumu ya timu za taifa kurejea kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo dhidi ya Horseed FC.

"Wachezaji wote wamerejea kambini akiwamo nyota wa nje ambao walikuwa katika majukumu ya mataifa yao, wanaendelea vizuri na tuko tayari kwa ajili ya kupambana kufutata matokeo chanya dhidi ya Horseed SC," alisema Zaka.

Aidha, Zaka alisema katika mchezo huo watamkosa straika wao hatari, Prince Dube ambaye ni majeruhi kwa sasa.

"Wachezaji wote wako salama, isipokuwa kwenye mechi hiyo tutamkosa Dube, ambaye alipata majeraha tukiwa Zambia kwenye kambi wakati wa mechi za kirafiki," alisema.

Baada ya mechi hiyo, mchezo wa marudiano umepangwa kuchezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, saa 10:00 jioni, na utahesabiwa kuwa ni wa ugenini kwa Azam na nyumbani kwa Horseed, ambayo imeomba ufanyike hapa nchini kutokana na hali ya machafuko kwa Somalia.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (watatu kushoto) na baadhi ya wawakilishi wa kampuni zilizodhamini mbio za NMB Marathon 2021 wakionyesha alama ya upendo inayoakisi kaulimbiu ya mbizo hizo ya 'Mwendo wa Upendo', wakati wa hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana ya kutangaza mgeni rasmi na wadhamini wa mbio hizo zitakazofanyika Septemba 25, mwaka huu. Wapili kulia ni Mkurugenzi wa Mikakati na Ukuaji wa Biashara Coca Cola Kwanza, Josephine Msaliwa (aliyevaa nyekundu) na katikati ni Mwakilishi wa Toyota, Nadah Dhiyebi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Waziri Mkuu mgeni rasmi NMB Marathon 2021*

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, amekubali kuwa mgeni rasmi na mshiriki wa mbio za NMB Marathon 2021, ambazo zimesogezwa mbele na sasa zitafanyika Septemba 25, mwaka huu, badala ya Septemba 18 kama iliyotangazwa awali wakati wa uzinduzi.

Hayo yamesemwa na Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa NMB, Filbert Mponzi, wakati wa hafla ya kutangaza wadhamini wa mbio hizo na 'kategori' zake, iliyofanyika makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam, ambako alisema idadi yao imefanya kupata makusanyo kiasi cha Sh. milioni 226, kati ya walizopanga kukusanya.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mponzi alisema wanamshukuru Waziri Mkuu Majaliwa kwa kukubali ombi lao la kuwa mgeni rasmi na mshiriki wa mbio hizo zenye lengo la kukusanya Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne, zitakazotumika kulipia gharama za matibabu ya kinamama wenye maradhi ya fistula kwenye Hospitali ya CCBRT.

Mponzi alibainisha kuwa, NMB imevutiwa mno na uungwaji mkono sio tu wa waziri mkuu kukubali ombi lao, bali pia kutokana na idadi kubwa ya kampuni na taasisi zilizojitokeza kudhamini, ili kufanikisha upatikanaji wa makusanyo ya kusaidia gharama za kutibu kinamama wenye maradhi hayo.

"Tunamshukuru na kumpongeza waziri mkuu kwa kukubali kuwa mgeni rasmi na mshiriki wa NMB Marathon chini ya kaulimbiu ya 'Mwendo wa Upendo,' ambazo sasa zitafanyika Septemba 25 badala ya 18 tuliyotangaza awali wakati tukizindua mbio hizi, mabadiliko yaliyolenga kuongeza muda wa usajili kama tulivyoombwa na washiriki watarajiwa.

"Shukrani za dhati pia ziwaendee kampuni na taasisi zilizoungana nasi kudhamini mbio hizi muhimu kwa ustawi wa afya za kina mama wenye Fistula nchini. Udhamini wao ni sapoti kubwa katika kukabiliana na changamoto ya maradhi hayo yanayotesa wanawake walio wengi ambao wanashindwa kumudu gharama za matibabu," alisema Mponzi.

Mponzi aliwataja wadhamini hao kuwa Kampuni za Bima za Sanlam na UAP ndio wadhamini wakuu wa kinyang'anyiro hicho kinachovuta hisia za wengi, huku Alliance Assurance wakiwa wadhamini wa 'kategori' ya Platinum.

Kampuni nyingine na kategori zao kwenye mabano ni Jubilee Insurance, Toyota Tanzania, Britam Insurance, Coca Cola, Reliance Insurance na Aris (Gold), Jubilee Life Insurance na Metro Life Assurance (Bronze), E Fm na Tv E (Media Partner) na SGA Security na Strategies Insurance.

# Michezo

Ijumaa Septemba 10, 2021

Nipashe




Real wamgeukia Lewandowski UKURASA 22

NIPO TAYARI...



Heritier Makambo. **PICHA: YANGA SC**

## Manara 'ajilipua' Simba kwa Yanga

**Na Tunu Hassan,** TUDARCo

LICHA ya kuhudumu kwa mabingwa wa nchi, Simba kwa kipindi kirefu akiwa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, amesema yeye hajawahi kuwa na mapenzi na timu hiyo, huku akitaka kwa sasa aulizwe mambo yanayohusu klabu yake ya Yanga pekee, anakofurahia maisha zaidi ya alikotoka.

Akizungumza na mwandishi wetu Dar es Salaam jana, Manara ambaye kwa sasa amehamia upande wa pili kuwa msemaji wa klabu hiyo, alisema katika maisha yake hajawahi kuwa Simba na kwamba yeye ni Yanga na kama kuna ukubwa aliwahi kuwaaminisha Wanasimba, basi huenda alikuwa amelewa.

"Moja ya kazi kubwa niliyoifanya labda ni kuonyesha ukubwa 'feki', hiyo dhambi nilitenda vibaya sana kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nipo tayari kuhukumiwa hata [kwenda] gerezani kwa kufanya ulaghai wa 'kufiksi' ukubwa ambao haupo," alisema.

Aliongeza kuwa Yanga ndiyo klabu kubwa na yenye mataji mengi zaidi vinginevyo ni uongo ambao yeye mwenyewe hapo nyuma alishiriki kuupika.

Alisema watu ambao wapo maalumu kwa ajili ya kumchafua, atawashughulikia vizuri kwa kuwa anajua kila kitu kinachoendelea.

Wakati Manara akisema hivyo, takwimu zinaonyesha kwa ujumla Simba ndiyo klabu iliyobeba makombe mengi (mara 51) yanayojulika nchini wakati Yanga inayoongoza kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu (mara 27 dhidi ya watani zao walioubeba mara 22), yenyewe kwa mataji yote kwa ujumla ikifanya ikibeba mara 48 pekee.

# Nabi awapa Makambo, Mukoko kazi maalum J'2

## ●●● Ni katika kuhakikisha Rivers United haichomoki kwa Mkapa, huku Kibwana naye...

**Na Saada Akida**

BAADA ya taarifa mbaya ya kuwakosa nyota wake watatu katika mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria Jumapili wiki hii, haraka Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amepata suluhisho na kutoa majukumu maalum ili kuhakikisha wanapata ushindi mnono katika mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Juzi Yanga iliweka wazi kuwa wamepokea taarifa kutoka Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), kuwa hawataruhusiwa kuwatumia wachezaji wao wa tatu, kiungo Mganda Khalid Aucho, beki wa kulia, Mkongomani Shabani Djuma na straika Fiston Mayele ambaye ni raia wa DR Congo, sababu ikiwa ni wote kuchelewa kupata Hati za Uhamisho wa Kimataifa, ITC.**

Hata hivyo, haraka Nabi amepata suluhisho la wachezaji hao baada ya kutumia muda wake mazoezini kwa kuwaandaa na kuwapa majukumu maalum, Heritier Makambo katika nafasi ya ushambuliaji na Mukoko Tonombe kwenye kiungo mkabaji.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka ndani ya kambi hiyo, Nabi amewapa majukumu baadhi ya wachezaji huku Mukoko akipewa majukumu mazito ambayo alikuwa akitarajiwa kupewa Aucho.

Mtoa habari wetu alisema kwenye safu ya ushambuliaji ambayo awali alipewa Mayele ambaye katika michezo miwili mfululizo ya kirafiki, ameonyesha uwezo mkubwa wa kucheka na nyavu, kazi hiyo sasa imeelekezwa kwa Makambo huku pia Yacouba Songne na Yusuf Athuman nao wakiwekwa sawa kwa kuongezewa makali.

"Djuma, Aucho na Mayele walikuwa kwenye mipango ya Kocha Nabi, lakini baada ya sakata la kutopata ITC ya nyota hao, mwalimu ameamua kuwapa majukumu wachezaji wengine.

"Kazi kubwa aliyotakiwa kufanya Aucho kwa namna inavyoonekana mazoezini ni wazi ataendelea nayo Mukoko ambaye yuko fiti, huku eneo la Djuma likibaki kwa Kibwana Shomari baada ya kufanya vizuri kwa msimu uliopita," alisema.

Kwa upande wa Msemaji wa Yanga, Haji Manara, alisema kuhusu kambi ya timu hiyo inaendelea vizuri, kuelekea mchezo huo na kwamba hawana presha kwa kukosekana kwa wachezaji hao kwa kuwa tayari Nabi amepata mbadala wa nyota hao watakaoikosa mechi hiyo.

"Kila kitu kinaenda vizuri na tayari kocha Nabi, anaendelea kufanya kazi yake, tunatarajia kupata matokeo mazuri na kusonga mbele kwenye michuano hiyo," alisema Manara.

Yanga itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Rivers United, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili kabla ya timu hizo kurudiana nchini Nigeria Septemba 18, mwaka huu.

Timu itakayopata matokeo ya jumla kwenye mechi hizo mbili, itakutana na mshindi wa jumla kati ya Al-Hilal ya Sudan na Fasil Ketema ya Ethiopia, ambazo nazo zitashuka dimbani Jumapili.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >